

**ULINGANISHI CHANGANUZI WA MOFU NJEO ZA KIKARA NA
KISWAHILI**


JANUARY PETER NYAWEMA MAGESA

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KUKAMILISHA MASHARTI YA
SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA ISIMU YA
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA, DAR ES SALAAM**

2017

UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI

Mimi J.S.Mdee, ninathibitisha kwamba nimesoma tasnifu hii iitwayo ‘*Ulinganishi Changanuzi wa Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili*’ na nimeridhika kuwa tasnifu hii imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa utahini wa Shahada ya Uzamili (M.A) ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.



Prof. James S. Mdee

(Msimamizi)

.....

Tarehe

HAKI MILIKI

Sehemu yoyote ya kazi hii ya Tasnifu hairuhusiwi kubadilishwa kwa ajili yoyote iwayo ya kietroniki, kunakilisha, kurudufu, katika hali yoyote, bila ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa Tasnifu hii au chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

TAMKO

Mimi, Magesa Peter Nyawema January, ninatamka na ninathibitisha kwamba, Tasnifu hii iitwayo **Ulinganishi Changanuzi wa Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili** ni kazi yangu mimi mwenyewe kwamba, haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kingine chochote kwa ajili ya kutunikiwa shahada yoyote.

.....

Saini

.....

Tarehe

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mama yangu Mecktrida Wegesa Nombe wa Ukerewe kwa kunipeleka shule. Pia mke wangu Sia Donath, kwa kunipa ushirikiano wa karibu katika kukamilisha shahada ya uzamili kwa kunitia moyo na kuniombea kwa Mungu nilipokuwa ninakata tamaa. Bila kuwa sahu wanangu Mercy, Metusela, Marcus na Mikayahu kwa kunivumilia muda wote ambao nilikuwa na fanya kozi hii kwa kukosa muda wa kuwa nao.

SHUKURANI

Kazi hii imekamilika kutokana na michango ya watu wengi walioshirikiana nami katika kufikisha kazi hii kama ilivyopangwa. Sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwa watu wote hao ambao walinisaidia katika kufikisha utafiti huu na kuuona hivi jinsi ulivyo. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mungu muumba mbingu na nchi kwa kunitia nguvu, uzima na kuniwezesha kukamilisha kazi hii na kuifikisha katika hatua hii kama inavyoonekana.

Pili, napenda kutoa kongole zangu kwa msimamizi wangu Profesa James Salehe Mdee amekuwa nami bega kwa bega katika kuhakisha kuwa utafiti huu unafanyika katika kiwango hiki.

Tatu, kongole zangu ziwaendee wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili katika chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa mchango wao walionipa: Prof. Mdee, Prof. Sengo, Prof. Mbogo, Dkt. Zelda, Dkt. Simpasa, Dkt. Lipembe, Dkt. Omary, na Dkt Mreta Mungu awape uzima na neema za kipekee ili waendeleo kutoa mchango wa kitaaluma kwa Taifa letu na nje ya nchi. Nne, shukurani zangu za dhati kwa wanafunzi wote wa shahada ya uzamili ya Kiswahili wa mwaka wa masomo 2014/2015.

Tano, shukurani zimwendee Mkurugenzi wa TATAKI Dkt. Mosha, E na Bi. Msighwa, E wa chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam kwa kunipa kibali kutumia Makavazi na Maktaba ya TATAKI. Bila kuwasahau David Simon Kilangi, Leonard Benard Kulwijira na Innocent Lukondo Mataba walionitajamali.

IKISIRI

Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza, kubaini na kulinganisha mofu njeo za kitenzi cha Kikara na za Kiswahili ili kujua idadi yake, mazingira zinapotokea na athari ya maumbo yake inayotokana na mazingira zilimo. Utafiti huu ulifanywa katika kata za Bukiko na Nyamanga wilaya ya Ukerewe kwa kuwatumia watoa habari 45 waliosailiwa na kujibu maswali. Utafiti huu umetumia nadharia ya Ulalo ya Reichenbach ambayo huchunguza, hubainisha na kulinganisha mofu njeo katika lugha ya Kikara na Kiswahili. Aidha nadharia hii inahusisha maumbo ya mofu njeo kwa kuonyesha wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao. Mbinu ya utafiti iliyotumika katika kukusanya data ilikuwa ni usaili na dodoso. Katika utafiti huu watoa taarifa waliteuliwa kwa kuzingatia kigezo cha usampulishaji lengwa na nasibu. Uchambuzi wa data ulibainisha kuwa lugha zilizochunguzwa zilikuwa na idadi tofauti ya mofu njeo. Kikara kina jumla ya mofu njeo saba ilihali Kiswahili kina mofu njeo tano. Utafiti huu uligundua mazingira ya kutokea kwa mofu njeo hizi katika vitenzi yalikuwa tofauti kwa baadhi ya mofu njeo na kufanana kwa mofu nyingine. Aidha maumbo ya mofu katika vitenzi yaliathiriwa na mazingira yalimokuwa, ambazo husababishwa na muungano wa irabu zinazokabiliana katika kingo zake.

YALIYOMO

UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI	ii
HAKI MILIKI.....	iii
TAMKO	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI	vi
IKISIRI	vii
UFUNGUO WA ISHARA NA VIFUPISHO	xii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xiv
ORODHA YA VIELELELZO.....	xv
SURA YA KWANZA.....	1
1.0 UTANGULIZI	1
1.1 Usuli wa Tatizo	2
1.2 Kauli Kuhusu Tatizo	7
1.3 Lengo kuu la Utafiti	8
1.3.1 Malengo Mahsusi	8
1.4 Maswali ya Utafiti	8
1.5 Umuhimu wa Utafiti.....	9
1.6 Mipaka ya Utafiti	9
1.7 Fasili ya istilahi zilizotumika katika kazi hii.....	10
1.8 Hitimisho	11
SURA YA PILI.....	12
2.0 MAPITIO YA MATINI ZINAZOHUSIANA NA MOFU NJEO	12
2.1 Utangulizi	12

2.2	Mofu Njeo	12
2.3	Pengo la Utafiti.....	39
2.4	Kiunzi cha Nadharia	40
2.4.1	Nadharia ya ulalo ya Reichenbach	40
2.5	Hitimisho	42
SURA YA TATU		43
3.0	USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI	43
3.1	Utangulizi	43
3.2	Usanifu wa Utafiti	43
3.3	Eneo la Utafiti	43
3.4	Mbinu za Utafiti	44
3.4.1	Usaili	44
3.4.2	Dodoso	44
3.5	Aina ya Data Iliyokusanywa	45
3.5.1	Data ya Msingi	45
3.5.2	Data ya Upili	45
3.6	Sampuli na Usampulishaji.....	46
3.6.1	Sampuli.....	46
3.6.2	Usampulishaji.....	46
3.6.3	Usampulishaji Lengwa	46
3.6.4	Usampulishaji Nasibu	47
3.6.5	Usampulishaji Makusudio.....	47
3.7	Uchambuzi wa Data	48
3.8	Ukusanyaji wa Data	49

3.9	Hitimisho	50
SURA YA NNE.....		51
4.0	UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA MOFU NJEO	
	ZA KIKARA NA ZA KISWAHILI.....	51
4.1	Utangulizi	51
4.2	Uwasilishaji wa Data.....	51
4.2.1	Nafasi ya Mofu Njeo Katika Kitenzi cha Kikara	52
4.2.2	Mofu njeo ya Kikara Wakati Uliopo (njeopo)	58
4.2.3	Mofu Njeo ya Kikara Wakati Ujao (Njeojao)	65
4.2.4	Mazingira ya Mofu Njeo na Jinsi Inavyoathiriwa na Umbo la Kitenzi cha Kikara	78
4.3	Nafasi ya Mofu Njeo Katika Kitenzi cha Kiswahili.....	86
4.3.1	Mofu Njeo za Wakati Uliopita	86
4.3.2	Mofu Njeo za Wakati Uliopo (Njeopo).....	90
4.3.3	Mofu Njeo za Wakati Ujao (Njeojao)	93
4.3.3.1	Nafasi ya Mofu Njeo ya Wakati Ujao Katika Kitenzi cha Kiswahili	94
4.3.4	Idadi ya mofu njeo za kitenzi cha Kiswahili	96
4.3.5	Mazingira ya Mofu Njeo na Jinsi Inavyoathiriwa na Umbo la Kitenzi cha Kiswahili	96
4.4	Kulinganisha mofu njeo za Kikara na Kiswahili	98
4.4.1	Nafasi ya mofu njeo katika kitenzi cha Kikara na Kiswahili.....	99
4.4.2	Idadi ya mofu njeo za Kikara na Kiswahili	103
4.5	Hitimisho	105

SURA YA TANO	107
5.0 MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO.....	107
5.1 Utangulizi	107
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti.....	107
5.3 Mchango wa Utafiti.....	109
5.4 Mapendekezo ya Tafiti Zijazo.....	109
5.5 Hitimisho	110
MAREJEO.....	111

UFUNGUO WA ISHARA NA VIFUPISHO

-	:	Mpaka wa mofu
()	:	Mabano ya jumla
/	:	Ni zote
/	/:	Uwasilishaji wa fonimu
{ }	:	Mabano ya mofu njeo
+	:	Ukiongeza
<	:	Inatokana na
>	:	Inakuwa
amm:		alama ya muda wa mazungumzo
amr:		alama ya muda rejelewa
amt:		alama wa muda wa tukio
Dkt:		Daktari
ir.mw :		irabu mwisho
kan:		mofu kanushi
ks:		kiambishi sioukomo
mr:		muda rejelewa
mt:		muda wa tukio
mz:		muda wa mazungumzo
mzz:		mzizi
nfs: nafsi		(1= kwanza, 2= pili, 3= tatu)
njeojao:		mofu njeo wakati ujao
njeopita:		mofu njeo wakati uliopita
njeopo:		mofu njeo wakati uliopo

Prof.: Profesa

TATAKI: Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili

Ts: kitenzi kisaidizi

um: umoja

wi: wingi

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1.1:	Mpangilio wa Mofu na Idadi	4
Jedwali 4.1:	Kusawazisha Matamshi Baina ya Irabu /a/ na / i / huzua irabu / e /	68
Jedwali 4.2:	Nafasi za Mofu Njeo Za Kitenzi Cha Kikara Na Kiswahili Zinapotokea Wakati Uliopita	99
Jedwali 4.3:	Nafasi ya Mofu Njeo za Kitenzi cha Kikara na Kiswahili Wakati Uliopo	100
Jedwali: 4.4:	Kufanana kwa Nafasi za Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Wakati Ujao.....	101
Jedwali 4.5:	Kufanana kwa Nafasi za Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Wakati Ujao Mofu Kanushi.....	101
Jedwali 4.6:	Tofauti ya Nafasi ya Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Wakati Uliopo Mofu Kanushi.....	102
Jedwali 4.7:	Tofauti ya Nafasi ya Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Wakati Ujao Mofu Kanushi	103
Jedwali 4.8:	Idadi ya Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Katika Wakati Uliopita	104
Jedwali 4.9:	Idadi ya Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Wakati Uliopo	104
Jedwali 4.10:	Idadi ya Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Wakati Ujao	105

ORODHA YA VIELELELZO

Kielelezo 2.1: Uwasilishaji wa Muda	12
Kielelezo 2.2: Uwasilishaji wa Muda	13
Kielelezo 2.3: Uwasilishaji wa Muda	13

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Utafiti huu unahusu uchunguzi wa mofu ya lugha ya Kikara na Kiswahili kwa lengo ya kuzilinganisha na kubaini idadi yake na mazingira zinamotokea katika vitenzi vya lugha hizi. Katika sura hii tunaeleza usuli wa tatizo, kauli kuhusu tatizo, lengo kuu la utafiti na malengo mahsusi ya utafiti. Aidha maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti huu kwa jumuiya ya akademika na kwa jamii na mipaka ya utafiti ni mambo yatakayoelezwa hapa pia. Kabla ya kufanya hivyo tutaeleza kwa ufupi kuhusu lugha ya Kikara na Kiswahili.

Kikara na Kiswahili ni lugha za Kibantu. Kikara ni lugha inayozungumzwa na Wakara wanaoishi katika kisiwa cha Ukara kilicho katika ziwa Viktoria. Kwa mujibu wa LOT, (2009) Kisiwa cha Ukara kina kadiliwa kuwa na wazungumzaji 114,990. Kisiwa hiki cha Ukara ni moja ya visiwa 21 vinavyounda wilaya ya Ukerewe. Lugha ya Kikara ambayo hujulikana pia kama Kiregi kwa mujibu wa Mekacha (2000) akimnukuu Nurse na Hinnebusch (1993) kipo katika kundi la E.25 Suguti ambalo hujumuisha lugha za Kijita, Kikwaya, Kiruri na Kikara chenyewe (Kiregi). Kiswahili ni lugha ya watu wa pwani na visiwa vinavyopakana na pwani ya Afrika Mashariki, lakini sasa imeenea nchi nzima ambapo inafahamika kama lugha ya kwanza na ya pili pia. Kwa mujibu wa uainishaji wa Guthrie (1948) Kiswahili kipo katika ukanda wa kijiografia wa G kundi la 40 namba G 42.

Mofu ni dhana ya mofolojia ambayo imechambuliwa na baadhi ya wanaisimu

mbalimbali katika mitazamo tafauti. Wanaisimu baadhi walioshughulikia mofu ni: Katamba na Stonham (2006) wanasema mofu ni umbo la nje linalowakilisha mofimu katika lugha. Habwe na Karanja (2007:74-76) wanaifasili mofu kama kipashio kidogo kabisa cha neno chenye kusitiri maana. Wanaendelea kusema kuwa uhusiano kati ya mofu na mofimu ni ule wa umbo na yaliyomo au kiashiria na kiashiriwa. Hata hivyo, kuna vitabu vingine vya isimu na mofolojia vimekuwa vikijadili zaidi mofimu na aina zake pamoja na alomofu bila kubainisha mofu. Rubanza (1996: 13-80) anasema mofimu ni kipashio kidogo kabisa cha kiisimu ambacho kina maana. Alomofu ni maumbo zaidi ya moja ambayo huwakilisha mofimu moja. Besha (1994:59-66) anasema mofimu ni vipashio vidogo sana vya msingi vinavyotumika katika kuunda maneno ya lugha. Wesana-Chomi (2013:7, 28) anasema kuwa mofimu ni kiambajengo cha neno, ni umbo lenye maana na ambalo linachangia muundo wa kimofolojia wa neno. Kuhusu alomofu Wesana-Chomi, (ameshatajwa) anasema kuwa ni maumbo tofauti yanayowakilisha mofimu moja yakiwa na maana ya mofimu hiyo hiyo.

Mdee (1999: 8) anasema kuwa mofimu ni kipashio kidogo kuliko vyote katika lugha chenye maana kisarufi. Anaendelea kusema kuwa mofimu ni kipashio kidogo kuliko neno na ndicho kinachojenga neno. Mfaume (1984:28) kwa upande wake anasema mofimu ni maumbo madogo kabisa ambayo yana maana na hayawezi yakagawika katika maumbo madogo zaidi yakaleta maana.

1.1 Usuli wa Tatizo

Mofu ni umbo la nje linalowakilisha mofimu katika lugha, (Katamba na Stonham

2006:24). Habwe na Karanja (2007:74-76) wanaifasili mofu kama kipashio kidogo kabisa cha neno chenye kusitiri maana. Wanaendelea kusema kuwa uhusiano kati ya mofu na mofimu ni ule wa umbo na yaliyomo au kiashiria na kiashiriwa.

Mfano 1:

a-na-lim-a

nfs- 3 um - njeopo- mzi-irabu mwisho

Katamba na Stonham (2006:24) wanasema kuwa mofu ni umbo la nje linalowakilisha mofimu katika lugha.

Mfano: 2

she- park- *ed* (park)

nfs 3um -mzi- njeopita

‘a - *li*- egesh- a’

Mofu imefasiliwa pia kama ni vipande vya neno ambavyo vimesetiri mofimu. (Mareale (1978) Kwa mujibu wa Mareale (keshatajwa) kila mofu ina maana maalumu inapokuwa katika neno.

Mfano: 3

a-na-imb-a (anaimba). Neno hili lina mofu nne na kila moja ina maana.

{a-} mofu nafsi ya tatu ya mtenda; umoja

{-na-} mofu njeo, wakati uliopo

{imb-} mofu mzizi wa neno

{-a} mofu dhamiri ya tendo

Fasili zote hizi zinafanana. Wanazuoni wote wanakubaliana kuwa mofu ni kipashio cha kimaumbo ambacho hakiwezi kugawanywa katika sehemu ndogo zaidi zenye kuleta maana. Kwa maana hii kila kiambishi ni mofu na kila mzizi wa neno ni mofu. Kama inavyoonekana katika jedwali la 1.1 hapa chini.

Jedwali 1.1: Mpangilio wa Mofu na Idadi

	Neno	Mofu						Idadi
a)	kalamu	kalamu	-	-	-	-	-	1
b)	alimpigia	a	li	m	pig	i	a	6

Chanzo: Mtafiti

Baada ya kueleza maana ya mofu, sasa tutafafanua mofu za njeo na jinsi zinavyojidhihirisha katika kitenzi. Mofu njeo kwa mujibu wa Crystal (1991:348) ni sehemu ya umbo la kitenzi ambalo huelezea umbo na muda unaolejerea taarifa. Lindfors (2003) anaieleza mofu njeo kama msimbo wa uhusiano nukuzi kati ya sehemu mbili za mhimili za mahali pa muda. O’Grady na wenzake (1997:733) wanaifasili mofu njeo kama kategoria ya kimofolojia ambayo hurejelea uhusiano kati ya wakati na muda wa mazungumzo. Kutokana na fasili hizi twaweza kusema kuwa, mofu njeo ni umbo la kimofolojia ambalo hurejelea uhusiano kati ya muda wa mazungumzo na tukio katika lugha.

Tafiti zilizofanywa kuhusu mofu njeo katika lugha za Kibantu ni chache. Baadhi ya tafiti hizo ni kama vile, Besha (1985) Mreta (1998), Beaudoin-Lietz (1999), Nurse (2008) na Walker (2013). Besha (1985) alishughulikia mfumo wa njeo na hali na kugundua kuwa lugha ya Kishambala ina mofu njeo nane na mofu hali moja. Mreta (1998) alichunguza mofu njeo na hali katika lugha ya Chasu na kugundua kuwa

lugha ya Chasu ina mofu njeo 7 na mofu hali 6. Beaudoin-Lietz (1999) alifanya utafiti juu ya miundo ya mofu njeo, hali na ukanushi katika uundaji wa vitenzi vya Kiswahili sanifu. Katika utafiti huu, aligundua kuwa Kiswahili kina mofu njeo 3 na mofu hali 7.

Nurse (2008) alichunguza mofu njeo na hali za Kibantu katika mapitio mbalimbali kwenye lugha 100 za Kibantu alizochunguza. Kwa mujibu wa Nurse (ameshatajwa) mofu njeo hizi alizigawa katika makundi matatu ya wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao. Lugha za kibantu zinatofautiana kimuundo na zipo katika viwango mbalimbali. Wakati uliopita una viwango kuanzia kiwango 1 hadi 5, wakati uliopo una mofu njeo kuanzia 1 hadi 2 na wakati ujao una mofu njeo kuanzia 1 hadi 4. Mofu njeo hizi ni: Mofu njeo za wakati uliopita katika viwango tofauti ni hizi: -á-, -a-, -ka-, -aka-, -li-, a...-ile, -iti, -i, e...í, hi-, -ku-, na a..-zu, sá-,

Baadhi ya mofu njeo za wakati uliopo katika Kibantu ni: -a-, -ma-, ø-, -ó- na mofu njeo wakati ujao katika viwango tofauti ni: ngá-, -ka-, -aku-, -la-, -laa-, -ra-, -ri-, - dzá-, - ci-...-e, -e- zinatofautiana kimuundo kama zitakavyofafanuliwa katika sura ya 2

Tafiti za kulinganisha mofu njeo za lugha mbili au zaidi tofauti ni chache sana. Baadhi ya tafiti linganishiza lugha mbili au zaidi zimehusisha lugha za Kibantu na lugha za kigeni kama alivyofanya O'Grady na wenzake (1997), Katamba na Stonham (2006:24-34,241) na Walker (2013).

O'Grady na wenzake (1997) walilinganisha lugha ya Kibemba (lugha yenye toni) na Kiingereza na kugundua kuwa lugha ya Kibemba ina mofu za njeo 6 ambazo ni: (-

àlí-) juzi,(-àlíí-) jana,(-àcí-) leo mofu njeo ijayo ambazo ni: (-ká-)kesho kutwa,(-kà) kesho, na (-léé-) leo baadaye.

Katamba na Stonham (2006:24-34,241) walichunguza na kulinganisha mofu njeo katika lugha ya Kiganda na Kiingereza na kugundua kuwa Kiganda kina mofu za njeo 3 ambazo ni:-li- (wakati ujao),-a- (wakati uliopita) na -ø- (wakati uliopo) au (mofu ya hali).

Mfano: 4

(a)Tu-*li*-laba vitabu

“tu-*ta*-ona vitabu”

(b) ba-*a*-laba kitabu

“wa-*li*-ona vitabu”

(c) (ba-ø-kola) bakola

“wa-na-fanya au

‘hufanya’

Hakuna hadi sasa utafiti wa kulinganisha mofu za njeo za lugha za Kibantu peke yake uliokwisha kufanywa unaofahamika. Utafiti tunaoufahamu wa kulinganisha mofu za njeo ni wa Walker (2013) ambaye alifanya utafiti wa kulinganisha mofu njeo na hali katika lugha ya Kiingereza, lugha ya Kiswahili na Kiikizu, Kizanaki, Kiikoma, Kikabwa na Kisimbiti ambazo zote ni lugha za mkoa wa Mara za kundi (40). Kwa mujibu wa mwanazuoni huyu mofu njeo za lugha hizi zipo 9 na mofu hali

zipo 4 kama zitakavyoelezwa katika sura ya 2. Mofu njeo hizi ziko katika mgawanyo ufuatao: yaani mofu njeo iliyopita ambayo ina kuwa katika nyakati nne tofauti kama ifuatavyo; mofu njeo iliyopita zamani, mofu njeo iliyopita jana, mofu njeo iliyopita leo ambayo inagawanyika katika nyakati mbili (zaidi ya masaa matano yaliyopita na dakika chache zilizopita). Mofu njeo iliyopo na mofu njeo ijayo ambayo ina nyakati nne tofauti kama ifuatavyo; mofu njeo ijayo kuanzia kesho kutwa, mofu njeo ijayo kesho, mofu njeo ijayo saa chache zijazo leo na mofu njeo ijayo ndani ya masaa mawili. Mofu njeo za lugha hizi zinatofautiana kimuundo kama zitakavyoelezwa katika sura ya 2.

Utafiti wa kulinganisha mofu njeo za Kikara na za Kiswahili kama lengo la utafiti huu linavyoeleza haujafanyika. Japokuwa Kikara na Kiswahili ni lugha za Kibantu mofu njeo zao zinaelekea kutofautiana kwa idadi na hata mazingira zinapotokea. Utafiti utakaoibua tofauti hizi ni muhimu kufanyika ili kuonyesha tofauti hizi za kiisimu katika lugha za Kibantu.

1.2 Kauli Kuhusu Tatizo

Kama ilivyoelezwa juu, utafiti wa kulinganisha mofu njeo na hali za lugha tofauti za Kibantu tunaoufahamu ni ule wa Walker (2013) ambaye alilinganisha njeo na hali ya lugha ya Kiikizu, Kizanaki, Kiikoma, Kikabwa na Kisimbiti za mkoa wa Mara kwa kuzilinganisha na Kiingereza na Kiswahili. Hizi lugha za Mara ni za kundi moja la E.40 na mfanano wake ni dhahiri. Lugha ya Kikara ipo katika kundi la (E.25) Suguti ambalo lina Kijita, Kikwaya, Kiruri na (Kiregi) Kikara.

Hakuna utafiti uliokwisha fanywa wa kulinganisha mofu njeo za lugha ambazo zipo katika makundi tofauti kama vile ya Kiswahili (G 42) na Kikara (E.25 Suguti) na kuonyesha tofauti na mfanano wa vipengele vya kiisimu katika lugha hizi ambavyo kama tulivyoeleza juu zina mwelekeo wa kutofautiana. Kwa hivyo kutokana na hali hii ni dhahiri kuwa kuna haja ya kuchunguza Kiswahili na Kikara ili kuona ni kwa kiasi gani kipashio hiki kinajidhihirisha katika lugha hizi.

1.3 Lengo kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza, kubainisha na kulinganisha mofu njeo za Kikara na za Kiswahili ili kujua idadi yake na mazingira zinapotokea.

1.3.1 Malengo Mahsusi

- Kuchunguza nafasi ya mofu njeo katika kitenzi cha Kikara na cha Kiswahili ili kuona mazingira zinamotokea.
- Kubainisha idadi ya mofu njeo za Kikara na za Kiswahili ili kubaini iwapo ni sawa au la.
- Kubaini mazingira ya mofu njeo na jinsi inavyoathiriwa na umbo la kitenzi ambamo mofu inatokea.
- Kulinganisha mofu njeo za Kikara na Kiswahili ili kuona iwapo zinatokea katika nafasi ile ile au la.

1.4 Maswali ya Utafiti

- Je mofu njeo za Kikara na za Kiswahili zikilinganishwa huonekana kuwa hutokea katika nafasi ile ile au la?

- Mofu njeo za Kikara na za Kiswahili hutokea katika mazingira gani katika kitenzi?
- Je Kikara na Kiswahili zina idadi sawa ya mofu njeo?
- Je mazingira ya mofu njeo za kitenzi cha Kikara na za Kiswahili zinaathiriwa na umbo la kitenzi?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu mkubwa katika isimu ya lugha za Kibantu. Umuhimu huo umo katika maeneo makuu manne:

Kwanza, utafiti huu unalenga kuwasaidia wanazuoni, walimu na wanafunzi wanaojifunza lugha za kibantu katika dhana za mofu njeo katika lugha za Kibantu.

Pili, matokeo ya utafiti huu yatasaidia watafiti wa baadaye watakaotumia kama rejeo katika isimu.

Tatu, utakuwa kichocheo kwa watafiti wengine hususani wazawa wa lugha hii kushawishika kutafiti na kuandika Makala na vitabu juu ya lugha hii kwa nia ya kuikuza, kuitunza, na kuimarisha ili kuipa hadhi.

Nne, mofu za njeo katika lugha ya Kikara haijachunguzwa na kuandikwa, kwa hali hiyo kazi hii itafanya hilo na kutoa mchango katika taaluma.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu una lengo la kulinganisha vipengele vya kimofolojia vya mofu njeo za Kikara na za Kiswahili tu. Utafiti huu hautashughulikia mofu nyingine za lugha hizi

kama vile mofu kanushi, mofu hali, mofu patanishi, mofu sharti, mofu rejeshi, mofu yambwa, na kadhalika.

1.7 Fasili ya istilahi zilizotumika katika kazi hii

alomofu ni maumbo tofauti yanayowakilisha mofimu moja yakiwa na maana hiyo hiyo.

mofu ni umbo la nje linalowakilisha mofimu katika lugha.

mofu njeo ni kategoria ya kimofolojia ambayo hurejelea uhusiano kati ya wakati wa muda wa mazungumzo.

njeo ni umbo la kimofolojia ambalo hurejelea uhusiano kati ya muda wa mazungumzo na tukio katika lugha.

wakati uliopita kitambo katika (Kikara) huelezea matendo yaliyotendeka au kutotendeka siku mbili kabla ya muda wa mazungumzo nakurudi nyuma kama juma, mwezi, miezi na miaka iliyopita.

wakati uliopita wa karibu katika (Kikara) hutumika katika kuelezea matendo yaliyotendeka au kutotendeka siku moja kabla ya muda wa mazungumzo.

wakati uliopo katika (Kikara) hutumika kuelezea matukio yanayotokea au hayatokei sambamba na muda wa mazungumzo.

wakati ujao kitambo katika (Kikara) hutumika kuelezea matukio yatatokea au hayatatokea kuanzia miaka miwili na kuendelea hadi miaka mingi ijayo baada ya muda wa mazungumzo.

wakati ujao kitambo kiasi katika (Kikara) hutumika kuelezea matukio yanayotokea au hayatokei kuanzia siku moja hadi mwaka mmoja baada ya mazungumzo.

wakati ujao wa karibu katika (Kikara) hutumika kuelezea matendo yatakayotendeka au kutokutendeka muda mfupi baada ya mazungumzo hadi masaa machache yajayo kabla ya siku inayofuata.

wakati uliopita katika (Kiswahili) hutumika kueleza kuwa tendo lilitendeka au halikutendeka kabla ya kutolewa kwa taarifa.

wakati uliopo katika (Kiswahili) hutumika kuelezea kuwa tendo linafanyika au halifanyiki wakati ule ule ambao tendo linaendelea kufanyika.

wakati ujao katika (Kiswahili) hutumika kueleza tendo ambalo litafanyika au kutofanyika katika wakati wote ujao.

1.8 Hitimisho


Sura hii ilitalii usuli wa tatizo, kauli kuhusu tatizo, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Sura inayofuata inaelezea mapitio ya matini zinazohusiana na mofu njeo. Mapitio yalipitiwa yalisaidia katika kufikia lengo la utafiti huu.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA MATINI ZINAZOHUSIANA NA MOFU NJEO

2.1 Utangulizi

Sehemu hii inabainisha maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada hii. Machapisho ambayo tumeyazingatia ni yale yanayoelezea dhana ya mofu, alomofu, mofu njeo na kiunzi cha nadharia. Tumetumia nadharia ya ulalo ya Reichenbach ambayo inasema kuwa muda unarejelea alama tatu ambazo ni muda wa mazungumzo, muda wa tukio na muda rejelewa. Nadharia hii inaonyesha alama tatu muhimu za kuzingatia wakati wa kuelezea mahusiano ya nyakati katika lugha. Alama hizi ni alama ya muda wa mazungumzo (mz) muda ambao usemi unatamkwa, alama ya muda wa tukio (mt) muda ambao tukio linatokea, na alama rejelewa (ar) alama ya wakati uliopo kati ya muda wa mazungumzo na muda wa tukio.




Kielelezo 2.1: Uwasilishaji wa Muda

Chanzo: Reichenbach (1947)

2.2 Mofu Njeo

Kama tulivyoeleza katika sura ya kwanza, mofu njeo ni sehemu ya umbo la kitenzi ambalo huelezea umbo na muda unaolejerea taarifa (Crystal 1991). Comrie (1985) anasema kuwa wakati unaweza kuwasilishwa na mstari mnyoofu, wenye wakati


uliopita upande wa kushoto na wakati ujao kulia.” Katika uwasilishaji wake, wakati uliopo (alama) O kwenye mstari mnyoofu.



Kielelezo 2.2: Uwasilishaji wa Muda

Chanzo: Comrie (1985)

Comrie (1985) anaeleza kuwa mchoro wa muda huwasilisha utoshelevu kwa kuelezea mofu njeo katika lugha ya mwanadamu. Kwa mujibu wa Lindfors (2003) nadharia ya Reichenbach ya mofu njeo ina sehemu mbili ambazo ni uhusiano mahali rejeshi (umr) na muda wa tukio (mt). Makosa yanayojitokeza katika (umr) inapendekeza kuwa ni tukio lililoambatana na muda wa mazungumzo (mz). Uhusiano huo umepangwa katika mfumo ufuatao:



Kielelezo 2.3: Uwasilishaji wa Muda

Chanzo ni kutoka Lindfors (2003)

Lindfors (ameshatajwa) hueleza kuwa njeo inajitokeza katika makundi makubwa matatu kama kielelezo hapo juu kinavyoonesha. Kwanza ni wakati uliopita, ambao tukio la muda lililotokea kabla ya muda wa mazungumzo, uliopo ambao tukio la muda linaendelea na mwisho wakati ujao ambao muda wa tukio hufuata muda wa mazungumzo kabla ya tukio.

Besha (1985:198-279) aliyefanya utafiti juu ya mfumo wa njeo na hali katika lugha ya Kishambala alibainisha mofu njeo 8 na mofu ya hali 1 katika Kishambala. Besha (ameshatajwa) ameonyesha kuwa wakati uliopita una mofu njeo 4 na mofu ya hali 1 ambazo zina uhusiano kwa karibu na muda wa mazungumzo. Ili kujua tofauti ya muda unaorejelewa, wazungumzaji sharti wawe na maarifa ya nyuma yanayofanana.

Mofu za njeo za wakati uliopita zinazofafanuliwa na vielezi vya wakati ni:

- a) - *iyé* jana
- b) -*za*-siku ya jana,
- c) -*á*- siku ile wakati uliopita na
- d) -*áá*-siku nyingi zilizopita zamani.

Kwa kutumia vielezi vya wakati kama vile; *ghulo* (jana), *ghulo nakiyo* (jana usiku), *lelo* (leo), *lelo makelo* (asubuhi hii), *zuzi* (siku kabla ya jana), *haya kale* (siku nyingi zilizopita), *kloi ushwelo* (jioni) katika Kishambala huonyesha wakati, kama mfano ufuatao:

Mfano: 1

- a) ti-di-*iyé* maboko (ghulo) ‘tulipika ndizi (jana)’ (njeo ya wakati uliopita)

- b) ti-*z*^á-dika maboko (ghulo) ‘tulipika ndizi (jana)’ (njeo ya wakati uliopita)
- c) t-*á*-dika maboko (uja mushi) ‘tulipika ndizi (siku ile) (njeo ya wakati uliopita)
- d) t-*áá*-dika maboko (uju mushi) ‘tulipika ndizi (siku ile zamani)’ (njeo ya wakati uliopita zamani)

Besha (ameshatajwa) amefafanua kuwa kuna mofu 3 zinazobainisha wakati uliopo ambazo ni: -*ø*-wakati uliopo -*ta*- wakati uliopo wa kawaida na -*aa*- wakati uliopo wa kuendelea. Kwa mfano

Mfano: 2

- a) (ivi aha) ni- *ø*-onda ghembe ‘(sasa hivi) ninatafuta jembe’ (njeo ya wakati uliopo)
- b) (ivi aha) uko nyumba-i ti-*ta*-dika manga ‘(sasa hivi) tuko nyumbani tunapika mihogo’ (njeo ya wakati uliopo)
- c) (ivi aha) (uko nyumbai) waghani w-*aa*-j-a ‘sasa hivi huko nyumbani wageni wanakula’ (njeo ya wakati uliopo)

Ameeleza kuwa wakati ujao una mofu nje moja ambayo ni: -*ne*- (kesho)-*nee*- (siku zijazo)

Mfano: 3

- a) *ne*-ti-dik-e (maboko) (keloi) ‘tutapika (ndizi) (kesho)’
- b) *nee*-ti-dik-e (maboko) (iyo mushi yeiza) ‘tutapika ndizi siku zijazo’

ne- ina tumia vielezi vya wakati vifuatavyo: mushi (mchana), ushwelo (jioni), keloi (kesho) na kishindo (siku baada ya kesho) na *nee*- ina tumia vielezi vya wakati vifuatavyo: iyo mushi yeiza (siku zijazo) iyo myezi yeiza (miezi ijayo) ayo mavuli

yaza (miaka ijayo) Mofu ya wakati uliopo wa kuendelea ambayo ni *-aa-* haina toni isipokuwa inafanana na ile ya wakati uliopita ambayo huwa ina toni juu *-áá-*.

Pamoja na hayo, Besha (ameshatajwa) anataja jana mara mbili inawezekana ni makosa ya kiuandishi. Maana ameeleza kielezi (juzi) lakini hajatoa mfano kuhusu juzi. Huenda mojawapo inahusika na juzi.

Katika utafiti huu, mtafiti alionyesha kuwa mofu njeo za wakati uliopita moja hutokea mwishoni mwa kitenzi kama kiambishi tamati.

Mfano: 4

ti-di-*iyé* maboko (ghulo) ‘tulipika ndizi (jana)

Mofu njeo tatu zilizobaki wakati uliopita hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi.

Mfano: 5

- a) ti-zà-dika maboko (ghulo) ‘tulipika ndizi (jana)
- b) t-à-dika maboko (uja mushi) ‘tulipika ndizi (siku ile)
- c) t-áá-dika maboko (uju mushi) ‘tulipika ndizi (siku ile zamani)

Katika wakati uliopo mofu njeo zote tatu hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali.

Mfano: 6

- a) ni- \emptyset -onda < ni-na-tafuta
- b) ti-ta-dika < tu-na-pika
- c) iii) w-aa-j-a < wa-na-kula

Katika wakati ujao mofu njeo hutokea mwanzoni mwa kitenzi kabla mofu nafsi.

Mfano: 7

- i) *ne-ti-dik-e* < *tu-ta-pika*
- ii) *nee-ti-dik-e* < *tu-ta-pika*.

Kwa mujibu wa Besha (ameshatajwa) kuna athari za kiisimu ambazo zinatokana na kudondoka kwa irabu / *i* / ya nafsi katika wakati uliopo na kudondoka kwa irabu / *i* / ya nafsi katika wakati uliopita.

Mfano: 8

- a) *ti + á-dika* > *t- á-dika* (uju mushi) ‘tulipika (siku ile)
- b) *ti + áá-dika* > *t- áá-dika* (uju mushi) ‘tulipika (siku ile zamani)
- c) *wi- + aa-j-a* > *w-aa-j-a* < *wa-na-kula* (wakati uliopo)

Mreta (1998) alichunguza mofu njeo na hali katika lugha ya Chasu. Katika utafiti wake alibaini kuwa lugha ya Chasu ina mofu njeo 7 na mofu hali 6.

Mfano 9: Mofu njeo wakati uliopita

- a) *é - ð- ie yó* (wakati uliopita leo)
nfs3 um- / njeojao- mzz- ir.mw leo
 ‘alikuja leo’
- b) *á- na- im- a ighuo* (wakati uliopita kuanzia jana)
nfs3 um/-njeopita- mara moja- mz-ir.mw jana
 ‘alilima mara moja jana’
- c) *é- im - ie ishamba lakwé* (wakati uliopita wa kawaida)

nfs3 um/-njeopita- mzz- ir.mw shamba lake

‘alilima shamba lake’

- d) é- im - íe he mghunda (wakati uliopita zamani kiasi)

nfs3 um/-njeopita- mzz- ir.mw ndani ya makaburi

‘alilima ndani ya makaburi’

- e) é-!kí- im - íe hé- mghunda (wakati uliopita zamani sana)

nfs3 um/-njeopita- mzz- ir.mw. ndani ya makaburi

‘alilima ndani ya makaburi zamani sana’

Katika wakati uliopita mofu njeo zote tano hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali.

Wakati uliopo katika Chasu una mofu njeo 2, ambazo ni: { - ø - } na { é- ra- }.

Katika wakati uliopo { - ø - } huonyesha tendo linaendelea muda wa mazungumzo.

Mfano: 10 Mofu njeo wakati uliopo

- a) é- ø - tóng- a yó (wakati uliopo ambao tendo linafanyika leo)

nfs3um njeopo mzz- ir. mw leo

‘anaenda leo’

- b) é- ø - tóng- a yaño (wakati uliopo tendo litafanyika kesho)

nfs3um njeopo mzz- ir. mw kesho

‘anaenda kesho’

- c) é - ra- im- a- ishamba lakwé (wakati uliopo unaendelea hajafikia kikomo)

nfs 3um bado- mzz- ir.mw shamba lake

d) ‘bado analima shamba lake’

Katika wakati uliopo mofu njeo hizi zote hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali.

Katika wakati ujao Chasu una mofu njeo 2 ambazo huonyesha tendo litatendeka baadaye.

Mofu njeo -ne- ya wakati ujao inaonesha tendo litatokea muda mfupi baada ya muda wa mazungumzo.

Mfano: 11

a) é- ne- im- a ishamba lakwé (wakati ujao baadaye baada ya mz)

nfs3 um -njeojao- mzz- ir.mw shamba lake

‘atalima shamba lake’

b) é- ne- im- a miŌi yeðie (wakati ujao siku nyingi zijazo)

nfs3 um -njeojao- mzz- ir.mw siku zijazo

‘atalima siku zijazo’

Mofu njeo -ra- huelezea tendo litakalotokea baadaye katika wazo fulani.

Mfano: 12

a) é- ra- ok-a mwalimu. (wakati ujao siku zijazo)

nfs3 um -njeojao- mzz- ir.mw mwalimu

‘atakuwa mwalimu’

b) é- ra- bá-a ngwii.

nfs3 um -njeojao- mzz- ir.mw

‘atakata kuni’

Katika wakati ujao pia mofu njeo hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali.

Kwa mujibu wa Mreta (ameshatajwa) kuna mambo matatu yanayojitokeza kati Chasu. Kwanza, maumbo ya kimofolojia yanayotumika katika mofu njeo kimaana hayaendi sawia na hali halisi ya kile kinachoelezwa na maumbo yanayotumiwa na mofu njeo. Hii ina maana kuwa mofu njeo {-ø -} ya wakati uliopo inatumika pia katika mofu hali. Katika Chasu mofu njeo {-ra-} inatumika wakati uliopo na ujao. Katika mfano 12b kuna maana mbili: maana ya kwanza inatokea katika wakati uliopo ‘bado anakata kuni’ na maana ya pili inatokea katika wakati ujao ‘atakata kuni’. Pili, katika kitenzi kunakuwa na maumbo mawili yanayoonesha mofu njeo. Mfano wakati uliopita mofu njeo.

{é-} huonesha wakati uliopita na {- ie} huonesha ukamilifu wa tendo lenyewe. Tatu, mofu hizi za njeo zinahusiano sana na vielezi kwa kurejea maana nyingine.

Kuna athari za kiisimu ambazo zinatokana na kitenzi husika kuwa na toni au kutokuwa na toni kwenye irabu ya mwisho / *íe* / katika wakati uliopita zamani kiasi na wakati uliopita wa kawaida irabu ya mwisho /- *ie* /.

Platt (1972) alichunguza umbo la vitenzi vyenye toni katika lugha ya Kikuyu. Katika utafiti wake alibaini kuwa lugha ya Kikuyu ina mofu njeo 4. Platt (ameshatajwa)

ameonyesha kuwa wakati uliopita una mofu njeo 1 inayojitokeza katika wakati uliopita wa muda mrefu na wakati uliopita wa muda mfupi. Katika wakati ujao una mofu njeo 3, wakati ujao wa karibu, wakati ujao kitambo kiasi na wakati ujao wa kitambo.

a) *Mofu njeo katika Kikuyu wakati uliopita hujitokeza katika wakati uliopita wa muda mrefu na wakati uliopita wa muda mfupi. íré*

i) *Mofu njeo iliyopita muda mrefu (–íré)*

Mfano: 13

i) o-tem-íré ‘u-li-kata’

ii) á-gÓr-íré ‘a-li-nunua’

ii) *Mofu njeo iliyopita muda mfupi (–íré)*

Mfano: 14

i) óḁondék-íré ‘a-li-shona’

ii) óniin-íré ‘a-li-naliza’

b) *Mofu njeo ijayo*

Mofu njeo ijayo imegawanyika katika nyakati tatu

i) *Mofu njeo ijayo wa karibu (-ré-, á)*

Mfano: 15

i) o – ré - niin - á > o-ré-niin-a ‘u-ta-maliza’

ii) a - ré- gor - á > a-re-gÓr-a ‘a-ta-nunua’

ii) *Mofu njeo ijayo kitambo kiasi (-ko-, -á)*

Mfano: 16

- i) [ó [ko[án ek á > okwánéká `utaeneza`
- ii) [ó [ko [đòndeká > ókóđondéká `utategeneza`

iii) *Mofu njeo ijayo kitambo muda mrefu (-ka-, -a)*

Mfano: 17

- i) o-ka-tem-á 'u-ta-kata'
- ii) a-ka-gór-a 'a-ta-nunua'

Katika utafiti huu tunaona kuwa mofu njeo ya wakati uliopita hutokea baada ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi tamati.

Mfano: 18

- i) áá-ndek-iré 'a-li-andik-a'
- ii) o-tem-iré 'u-li-kata'

Katika wakati ujao mofu njeo hutokea kabla ya mzizi kama kiambishi awali.

Mfano: 19

- i) a - ré- gor - á > a-re-gór-a 'a-ta-nunua'
- ii) [ó [ko [đòndeká > ókóđondéká `utategeneza`
- iii) a-ka-tem-á 'u-ta-kata'

Athari inayoonekana ya kiisimu ambayo inasababishwa na msigano wa sauti za irabu zinapofuatana katika mofu njeo ijayo kitambo kiasi.

Mfano: 20

[ó [ko [áneká > okwáneká.

Aidha anaeleza kuwa, athari za kiisimu hujitokeza pale ambapo mofu njeo ambayo ina irabu yenye toni ya juu inapokaribiana na mzizi wa kitenzi ambao huanza na irabu husababisha irabu yenye toni kudondosha toni na irabu iliyo katika mzizi hupokea toni.

Mfano: 21

i) a- *ré-* gor- *á* > areg**óra** ‘a-ta-nunua’.

Walker (2013) alifanya utafiti wa kulinganisha njeo na hali katika lugha ya Kiingereza, Kiswahili na Kiikizu, Kizanaki, Kiikoma, Kikabwa na Kisimbiti ambazo zote ni lugha za mkoa wa Mara za Kundi E.40. Kwa mujibu wa mwanazuoni huyu mofu njeo zipo 9 na mofu hali zipo 4.

a) *Mofu njeo iliyopita*

Mofu njeo iliyopita ipo katika viwango vinne tofauti.

i) *Mofu njeo iliyopita zamani*

Mofu njeo *-ka-*, hutumika katika Kiikizu na Kizanaki, *-a (a)* - hutumika katika Kikabwa na Kisimbiti na Kiikoma haijaoneshwa na mtafiti wa kazi hii.

Mfano: 22

i) Kizanaki: tu-*ka*-gaamb-an-a na-we (ekare) `tuliongea naye (zamani) `

ii) Kisimbiti: (n-kare) tw-*aa*-shumaash-ire na-we. `Tuliongea naye (zamani) `

iii) Kikabwa: tw-*a*-hair-a na-we (akare). `Tuliongea naye (zamani) `

iv) Kiikizu: tu-*ka*-gaamb-an-a na-wi (ikari).` tuliongea naye (zamani) `

ii) *Mofu njeo iliyopita jana*

Mofu njeo *-ka-*, hutumika katika Kiikizu na Kizanaki, *-a (a)* - hutumika katika Kisimbiti, Kikabwa hutumia *-a-* na Kiikoma haijaoneshwa. (Walker 2013) alitoa mfano 1 wa Kikabwa (uk 44) kama ilivyo katika mfano 23 hapo chini.

Mfano: 23

Kikabwa: tw-*a*-bhin-iri (ejo) `tulicheza (jana)

(iii) *Mofu njeo iliyopita leo*

Mofu njeo iliyopita leo and Mofu njeo iliyopita inayotokea muda mfupi ndani ya masaa mawili tangu muda wa mazungumzo. Katika lugha hizi tano inajitokeza katika Kikabwa na inatumia vielezi vya wakati (nyenkya inu) (asubuhi hii).

Mfano: 24

i) Tu-bhin-iri nyenkya i-nu. “tulicheza asubuhi hii”

Walker (ameshatajwa) anasema kitu kimoja ambacho ni kigumu kabisa katika uthibitishaji wa usemaji juu ya wakati uliopita leo katika Kiswahili ni kweli kuwa maelezo ni yale ya wakati uliopita kuanza masaa mawili leo ambayo kiuhalisia inatokana na mofu ya hali *-me-*. Hii ni kwa sababu uhusiano wa mofu hali katika Kiswahili ni vigumu kutambua kama umbo la *-me-* linakuwa katika mofu njeo kwani uthibitishwaji wake upo katika mofu za hali. Anaendelea kusema kuwa, huu ni utata ambao hakuna uthibitishaji wa usemaji kutoka katika Kiswahili kwani ni vigumu sana kutofautisha aina hizi katika lugha nyingi za Kibantu (Nurse 2008: 94-99).

b) *Mofu njeo iliyopo.*

Mofu njeo iliyopo ina mofu njeo zifuatazo kulingana na lugha husika.

Mfano: 25

- i) Kikabwa: tw-aa-gy-a Darisaraamu `` tunaenda Dar-ES salaam” (wakati uliopo)
- ii) Kiikizu: tw-aa-j-a Daresaraamu `` tunaenda Dar-ES salaam” (wakati uliopo)
- iii) Kiikoma:to-ø- gha-ye Darisaraamu `` tunaenda Dar-ES alaam” (wakati uliopo)
- iv) Kisimbiti:to-ra-y-a Daresaramu`` tunaenda Dar-ES salaam” (wakati uliopo)
- v) Kizanaki: tu-ra-gy-a Darisaraam`` tunaenda Dar-ES salaam” (wakati uliopo)

c) *Mofu njeo ijayo*

Mofu njeo ijayo imegawanyika katika nyakati nne ambazo ni: leo ndani ya masaa 2 yajayo, baadaye leo, kesho na kesho kutwa na kuendelea.

i) *Mofu njeo ijayo kuanzia kesho kutwa*

Mofu njeo ijayo ambayo inatokea kuanzia kesho kutwa na kuendelea ni zifuatazo: Kiikizu na Kizanaki kinatumia -ra-, Kiikoma kinatumia -ko- na Kikabwa na Kisimbiti kinatumia -ri-

Mfano: 26

Kizanaki: Tu-ra-keranh-a na-we o-mwaka gu-no gu-kuz-a.

‘Tutaongea naye mwaka ujao’

Kiikizu: Tu-ra-gaamb-an-a na-wi u-mw-aaka gu-nu gu-ku-uz-a.

‘Tutaongea naye mwaka ujao’.

Kiikoma: N-to-*ko* -siiker-a na-we mo-mo-oka u-no o-ku-uch-a.

‘Tutaongea naye mwaka ujao.’

Kisimbiti: O-mo-oka ghu-yö ghu-ku-ush-a n-tu-*ri*-shumaash-a nawe.

‘Tutaongea naye mwaka ujao.’

Katika lugha hizi tano za Mara ni lugha mbili tu ambazo ni Kikabwa na Kisimbiti ambazo mofu njeo ni –ri-

(ii) *Mofu njeo ijayo kesho*

Mofu njeo ijayo inatokea katika matukio yanayotegemea kutokea kesho. Katika Kiikizu na Kizanaki hutumia –*ra*-, Kiikoma hutumia –*ko*-, Kikabwa –*aka*- na Kisimbiti hutumia –*ri*-.

Katika lugha hizi tano za Mara, Kizanaki na Kiikizu ndizo zinatumia –*ra*- lugha tatu zinazobaki kila moja ina mofu njeo yake.

Mfano: 27

Kikabwa: Tw-*aka*-hair-*e* na-we ejo. ‘Tutaongea naye kesho.’

Kizanaki: Izo tu-*ra*-keranhia nawe. ‘kesho tutaongea naye’

Kiikoma: N-to-*ko*-siikera nawe. ‘tutaongea naye’

Kisimbiti: N-tu-*ri*-shumaasha nawe. ‘tutaongea naye’

Kiikizu: Tu-*ra*-gaamb-an-a nawi. ‘tutaongea naye’

(iii) *Mofu njeo ijayo saa chache zijazo leo*

Mofu njeo ijayo saa chache zijazo leo ni tukio linalotegemea kutokea saa chache zijazo tangu muda wa mazungumzo.

Kiikizu na Kizanaki hutumia *-ra-*, Kiikoma hutumia *-ko-* , na Kikabwa na Kisimbiti hutumia *-aka-*.

Mfano: 28

Kisimbiti: Mo-ghorobha n-tw-*aka*-shumaash-e na-we. 'Tutaongea naye jioni hii.'

Hakuna mfano mwingine uliotolewa na mtafiti wa kazi tangulizi katika lugha zingine (walker 2013: 46)

iv) *Mofu njeo ijayo leo ndani ya masaa mawili*

Mofu njeo ijayo leo ni tukio linalotegemea kutokea ndani ya muda wa masaa mawili yajayo tangu muda wa mazungumzo lakini tukio hutokea kama ilivyopangwa. Hii ni katika Kisimbiti na Kikabwa (Mwita 2008: 47). Katika Kiikizu na Kizanaki hutumia *-ra-*, Kiikoma hutumia *-ko-* , na Kikabwa na Kisimbiti hutumia *-raa-*.

Mfano: 29

Kisimbiti: Ha-no se-raa-het-e se-dakika i-kömi n-to-*raa*-shumaash-e na-we.

'Tutaongea naye baada ya dakika kumi.'

Katika utafiti huu wa ulinganishi wa mofu njeo na hali katika Kiingereza, Kiswahili na lugha tano za mkoa wa Mara zilizo kundi (40) yaani, Kiikizu, Kizanaki, Kiikoma, Kikabwa na Kisimbiti, Walker (2013) anasema, mofu njeo za wakati uliopita zinatofautiana kimuundo. Lugha zilizo kusini mwa Mara ni: Kiikoma, Kiikizu, na Kizanaki na zilizo kaskazini ni: Kikabwa na Kisimbiti.

Katika mofu njeo iliyopita zamani, jana na leo Kiikizu na Kizanaki zinatumia mofu *-ka-* ilhali Kikabwa na Kisimbiti zinatumia mofu *-a(a)-* zamani na jana bali Kiikoma

kinatumia *-iri*. Katika utafiti (Walker 2013) pamoja na kueleza kuwa Kiikoma kinatumia *-iri* hakuna mfano wowote uliotolewa kuthibitisha alichoeleza.

Kizanaki na Kisimbiti zinatumia mofu njeo *-ra-*, Kiikizu na Kikabwa zina mofu *-aa-* na Kiikoma kina mofu njeo *-ø-* katika wakati uliopo. Wakati ujao Kiikoma, Kiikizu na Kizanaki zinatumia mofu njeo *-ra-*, Kikabwa na Kisimbiti zinatumia mofu njeo 3 ambazo ni *-raa-*, *-aka-* na *-ri-*.

Athari inayoonekana katika lugha hizi ni kuwa, mofu njeo *-aa-* ya wakati uliopita katika lugha ya kizanaki hutumika pia wakati uliopo katika lugha ya Kikabwa na Kiikizu. Mofu njeo *-ra-* ya wakati ujao katika lugha ya Kiikizu na Kizanaki hutumika pia wakati uliopo katika lugha ya Kizanaki na Kisimbiti.

Beaudoin-Lietz (1999) alifanya utafiti juu ya miundo ya mofu njeo, hali na ukanushi katika uundaji wa vitenzi vya Kiswahili sanifu. Mtafiti huyu alitumia uchanganuzi mofosemantikia na nadharia ya Guillaumian ilitumika katika kazi hii. Katika utafiti wake amesema kuwa katika Kiswahili sanifu mofu njeo hutokea kabla ya mzizi, hii ni tofauti na lugha nyingine za Kibantu. Katika kazi yake hii amebainisha kuwa Kiswahili kina mofu njeo 3 na mofu hali zipo 7.

Mofu njeo ya wakati uliopita unaonekana wazi kuwa tendo linaloelezewa limepita.

Mfano: 30

a) wa- li- imb- a (wakati uliopita katika uyakinishi)

nfs3um-njeopita-mzz- ir.mw

b) ha- wa- ku- imb- a (wakati uliopita katika ukanushi)

kan- nfs3um- njeopita- mzz- ir.mw

Mofu njeo ya wakati ujao tukio lake halijakuwepo au halijafanyika.

Mfano:31

a) wa- ta- imb- a

nfs3um-njeojao- mzz- ir.mw

b) ha- wa- ta- imb-a (wakati ujao katika ukanushi)

kan- nfs3um-njeojao- mzz- ir.mw

Katika kazi yake, Beaudoin-Lietz ameonyesha kuwa mofu *-na-* ni miongoni mwa mofu hali katika lugha ya Kiswahili. Katika utafiti huu mtafiti alitofautiana naye (tazama 4.3.2) kwa kuiona mofu hii kama mofu katika wakati uliopo. Katika utafiti huu umechangia katika isimu ya lugha kwa kutambua kuwa nafasi ya mofu njeo za Kiswahili sanifu hutokea kabla ya mzizi, pia mtafiti litamsaidia sana kwa sababu ni mojawapo ya lengo mahsusi la kuchunguza nafasi ya mofu njeo. Ingawa hivyo, bado kazi hiyo haikukidhi haja iliyokusudiwa na utafiti huu.

Nurse (2008) alichunguza mofu njeo na hali za Kibantu katika lugha 100 za Kibantu. Katika utafiti wake aligundua kuwa katika lugha za kibantu mofu njeo zake zina tofautiana katika viwango. Kwa mfano, zipo lugha ambazo wakati uliopita una viwango vitano. Wakati uliopita kitambo sana, wakati uliopita kitambo, wakati uliopita kitambo kiasi, wakati uliopita wa karibu na wakati uliopita wa karibu kiasi. Tuangalie mfano 32 lugha ya Kikongo-zombo hapa chini.

Mfano:32

Kikongo-Zombo

a) Wakati uliopita kitambo sana

tú- ø -súmba / tú-ø-súmb-idi / tu- ø -súmb-id-il-ing-i

‘tulinunua’ (wakati uliopita zamani sana)’

b) Wakati uliopita kitambo

tu- ø -súmba

‘tulinunua’ (muda uliopita kuanzia miezi miwili hadi miaka miwili)

c) Wakati uliopita wa karibu

tu- ø -súmb-idi

‘tulinunua’

d) Wakati uliopita wa karibu kiasi

tu- ø -sumb-idi

‘tulinunua’ (leo)

e) Wakati uliopita wa karibu

tu- ø -fuma-sumb-i au (tu- ø -fuma sumb-i)

‘tumenunua’ (leo baada ya muda wa mazungumzo)’

Pia zipo lugha zenye viwango vinne katika wakati uliopita. Viwango hivi ni: wakati uliopita kitambo, wakati uliopita kitambo kiasi, wakati uliopita wa karibu na wakati uliopita wa karibu kiasi. Tuangalie Mfano 33 katika Kinomaande hapa chini.

Mfano: 33

Kinomaande:

- a) Wakati uliopita kitambo
 tɔ-ŋ a-sɔsɔmb-ák-a (siku nyingi)
 ‘ulificha’
- b) Wakati uliopita kitambo kiasi
 nɔ-ŋa-nɔ námb-ak-a (zamani jana)
 ‘ulificha’
- c) Wakati uliopita wa karibu
 e- ŋ’á-meta’g-ák-a (mapema leo)
 ‘nilizungumza’
- d) Wakati uliopita wa karibu kiasi
- e) tɔ-ma-sɔ lɔgɔk-ɔ (saa chache zilizopita)
 ‘tulikuika’

Mofu njeo za wakati uliopita, lugha za kibantu zenye viwango vitatu ambavyo ni: wakati uliopita kitambo, wakati uliopita kitambo kiasi na wakati uliopita wa karibu. Tuangalie Mfano 34 katika Kipimbwe hapa chini.

Mfano: 34

Kipimbwe:

- a) Wakati uliopita kitambo
 tw-á-lí tu-g’ud-ile
 ‘tulinunua’
- b) Wakati uliopita kitambo kiasi
 (tw-á-lí) tu-ká-gud-íle

‘tulinunua’

c) wakati uliopita wa karibu kiasi

(tw-a-ti) tu-gud-ile

‘tulinunua’

Mofu njeo wakati uliopita, lugha za kibantu zenye viwango viwili ambavyo ni: wakati uliopita kitambo na wakati uliopita karibu. Tuangalie Mfano 35 katika lugha ya Kikundi hapa chini.

Mfano: 35

Kikundi

a) fu-dza-gula

‘tu/linunua’ (wakati uliopita jana na kuendelea)

b) f-á-gula

‘tu/linunua’ (wakati uliopita leo baada wa muda wa mazungumzo)

Nurse (ameshatajwa) anasema katika Kiswahili mofu njeo –li- na –ta- zinaonesha wakati uliokamilika lakini wakati uliopo mofu –na- hauna wakati asili bali hutegemea mofu njeo iliyo katika maneno. Wakati uliopo katika lugha nyingi za Kibantu hazina mofu za kipekee zinazoonesha wakati uliopo. Tuangalie Mfano 36 katika Kiduala hapa chini ambayo inawakilisha lugha zingine. Katika Kiduala wakati uliopo unaelezwa kwa kutofautisha mofu njeo zinazowekwa kwenye vitenzi ila ni wakati uliopo.

Mfano: 36

Kiduala

- i) na-*ma*-bol-a ‘ni-na-to-a’
- ii) na- \emptyset -bol-a ‘ni-na-to-a’ (rudia kutoa)
- iii) ná- \emptyset -bol-a ‘ni-na-to-a’ (rudia kila siku kutoa)
- iv) na-*Ó*-bol-a ‘ni-na-to-a’ (kutoa muda huo huo)

Wakati ujao katika lugha za Kibantu zifuatazo ni mofu njeo zinazotumika ambazo ni:

-ngá-, -ka-, -aku-, -la-, -laa-, -ra-, -ri-, - dzá-, - ci-...-e, -e-

Katika Mfano 37 hapa chini ni baadhi ya lugha za Kibantu zilizotumia hizo mofu njeo.

Mfano: 37

Kiswahili: wa-*ta*-zungumza

Kilucazi: tu-*ka*-ímb-a ‘ataimba’

Kimbundu: tu-*ka*-land-a ‘tutanunua’

Kikele: tó-*la*-kol-aka ‘tutafanya kazi

Kiruri: ci-*laa*-gul-e ‘tutanunua’

Kichewa: a-*dzá*-fik-a ‘atakuja’

Kimwera: ci-*tu*-o-lim-e ‘tutalima’

Kinyoro: tu-*ra*-gúr-a ‘tutanunua’

Kinyoro: tu-*ri*-gúr-a ‘tutanunua’

Kilamba: tw-*aku*-cit-a ‘tutafanya’

Katika wakati ujao pia lugha za kibantu zipo ambazo zina viwango vinne. Wakati wakati ujao kitambo, wakati ujao kitambo kiasi, wakati ujao wa karibu na wakati ujao wa karibu kiasi. Tuangalie mfano 38 lugha ya Kisena hapa chini.

Mfano: 38

Kisena:

a) Wakati ujao kitambo

ndi-na-ti ndi-dy-e

‘nitasema’ (wakati ujao wa kitambo)

b) wakati ujao kitambo kiasi

ndi-na-dya

‘nitakula’

c) wakati ujao wa karibu

ndi-sa-funa ku-dya

‘nitataka’

d) wakati ujao kiasi

ndi-na-dza ka-dya

‘nitakwenda kula’

Katika lugha za Kibantu zipo zenye viwango vitatu vya wakati ujao ambavyo ni: wakati ujao kitambo, wakati ujao kitambo kiasi na wakati ujao wa karibu. Tuangalie Mfano 39 katika Kipimbwe hapa chini.

Mfano: 39

Kipimbwe:

a) Wakati ujao kitambo

tu-lu-gul-ánga

‘tutanunua’ (mwezi ujao nakuendelea)

b) Wakati ujao kitambo kiasi

tu-lu-gul-á

‘tutanunua’ (kesho hadi mwezi ujao)

c) Wakati ujao wa karibu

tu-gud-ile

‘tutanunua’ (leo)

Mofu njeo wakati ujao, lugha za kibantu zenye viwango viwili ambavyo ni: wakati ujao kitambo na wakati ujao wa karibu. Tuangalie Mfano 40 katika lugha ya Kimatumbi hapa chini.

Mfano: 40

Kimatumbi

a) Wakati ujao Kitambo

n-aa-lúwa-t´uumuka

‘nitaanguka’

b) Wakati ujao wa karibu

ni-luwa-t´uubuka

‘nitaanguka’

Nurse (ameshatajwa) anasema mofu njeo za lugha za Kibantu hutokea kabla ya mzizi na nyingine baada ya mzizi katika kitenzi.

Tuangelie Mfano 41 hapa chini katika ya lugha ya Kipogolo na Kichiriku.

Mfano: 41

Kipogolo:

tu- ø- hemer-iti

nfs1wi-mofu kapa-mzz- njeopita

‘tulⁱnunua’

Kidchiriku:

ngá- tu- ø- ping-a

njeojao -nfs 1 wi - mofu kapa- mzz- ir.mw

‘tutarithi’

Baadhi ya mofu njeo katika lugha za Kibantu hutokea kabla ya kitenzi na wakati huo huo hutokea baada ya mzizi. Tuangelie pia Mfano 41 katika lugha ya Kiyanzi na Kilunda hapa chini.

Mfano: 42

i) Kiyanzi (n´e)- e- s- í

nfs2um njeopita-mzz-njeopita

‘uliweka’

ii) Kilunda: hi- tu- ku-y-a

njeojao-nfs1wi-njeojao-mzz-ir. Mw

‘tutaenda’

Mofu njeo huleta tofauti katika wakati kutokana na toni zinazojitokeza katika kitenzi. Tuangalie Mfano 43 katika lugha ya Kinyali, Kiewondo na Kiumbundu hapa chini.

Mfano: 43

i) Kinyali: k-á-kora ‘tulinunua’ wakati uliopita

k-á-korá ‘tunanunua’ au ‘tutanunua’ wakati uliopo au wakati ujao.

ii) Kiewondo: ma-á-dí ‘nilikula’ wakati uliopita

m-á-dí ‘ninakula’ wakati uliopo

iii) Kiumbundu: tw-á-land-éle ‘tulinunua’ wakati uliopita siku nyingi

tw-á-land-á ‘tulinunua’ wakati uliopita hivi karibuni

Nurse (ameshatajwa) kazi hii inaonyesha mchango katika utafiti huu, kwani kuna lugha za kibantu ambazo mofu njeo hutokea kabla ya mzizi na zipo zinazotokea baada ya mzizi.

Athari inayoonekana katika lugha hizi ni kuwa, mofu njeo –á- ya wakati uliopita katika lugha ya Kinyali hutumika pia wakati ujao katika lugha hiyo ya Kinyali, pia hutumika wakati uliopita katika lugha ya Kiewondo. Katika utafiti wa Nurse tunaona athari inayotokea ni kuwa toni zina athari mofu njeo na kuleta maana nyingine katika kitenzi husika. Kwa mfano mofu njeo iliyo katika kitenzi ‘madi’ inakuwa “ma-á-dí ” ‘nilikula’ wakati uliopita inakuwa “ m-á-dí ” ninakula wakati uliopo.

Mofu njeo –na- wakati uliopo lugha ya Kiswahili hutumika katika lugha ya Kisena katika wakati ujao.

Wesana-Chomi (2001, 2003) na amesema wakati ni sifa ya kitenzi ambayo huonesha wakati wa kufanyika kwa tendo au jambo. Anasema kuwa Kiswahili kina nyakati tatu na kila moja inaoneshwa kwa viambishi awali katika vitenzi. Katika kazi yake ameonesha mofu njeo 7 na mofu hali 5. Kwa mujibu wa Wesana – Chomi (ameshatajwa) wakati uliopo una mofu njeo 1 ambayo ni: {-na-}, wakati uliopita una mofu njeo 4 ambazo ni: {-me-}, {-li-}, {-ka-} na {-ku-} na wakati ujao una mofu njeo 2 ambazo ni: {-ta-} na {-taka-}. Tuangalie Mfano 44 hapa chini.

Mfano: 44

Kiambishi	Wakati	Mifano
-na-	wakati uliopo	<i>anasoma, anapika</i>
-ta-	wakati ujao	<i>atasoma, atapika</i>
-taka-	wakati ujao katika vitenzi rejeshi	<i>nitakaporudi</i>
-me-	wakati uliopita muda mfupi	<i>amepika, ameoga</i>
-li-	wakati uliopita muda mrefu	<i>alikwenda sokoni</i>
-ka-	wakati uliopita katika mfululizo wa matendo	<i>nikanunua samaki nikarudi</i> <i>Nyumbani nikapika,</i> <i>nikala halafu</i> <i>nikapumzika.</i>
-ku-	wakati uliopita katika vitenzi kanushi	<i>hakusoma, sikusoma</i>

Katika uainishaji huu wa Wesana – chomi una kasoro zifuatazo: Kwanza, kuunganisha mofu njeo {-ta-} pamoja na mofu rejeshi {-ka-} na kuisema ni mofu nje ya wakati ujao

{-taka-} kawaida mofu njeo hutokea moja tu katika kitenzi cha Kiswahili. Katika neno hili -taka- si mofu njeo bali ni kidahizo. Pili, uainishaji mofu hali {-me-} kuwa ni mofu njeo ya wakati uliopita siyo sahihi. Katika mfano wake wa mofu hali hauoneshi tofauti ya wakati uliopita na hali timilifu. Katika kazi yake ametoa mfano ufuatao: ‘mama amefua nguo’ kwa mujibu wa Wesana- Chomi hii ni mofu hali lakini amepika au ameoga anasema ni mofu njeo ya wakati uliopita. Tatu, mofu {-ka-} hutumika katika usimulizi wa matukio yanayojitokeza kwa kufuatana hii siyo mofu njeo ya wakati uliopita.

Kwa hiyo, katika utafiti huu tutaeleza zaidi katika sura ya nne juu ya mofu njeo (tazama 4.3.2).

Kutokana na kazi hizi tangulizi mtafiti alikuwa na shauku ya kufanya utafiti katika kipengele cha mofu njeo peke yake maana wanaisimu hawazitofautishi na mofu hali.

2.3 Pengo la Utafiti

Kutokana na mapitio hayo mbalimbali mtafiti ameona kuwa, tafiti nyingi zimeelezea kuhusu mofu njeo na hali. Ulinganishi wao ulijikita katika mfumo wa mofu njeo na hali, mofu njeo na hali au kazi yoyote iliyofanywa ikihusisha mofu njeo za lugha za Kibantu. Katika tafiti hizi hakuna zilizoelezea kuhusu ulinganishi changanuzi wa mofu njeo za lugha za makundi tofauti ya Kibantu kama vile Kikara na Kiswahili. Hivyo basi, ni lengo la utafiti huu kufanya ulinganishi changanuzi wa mofu njeo za Kikara na Kiswahili.

2.4 Kiunzi cha Nadharia

Katika sehemu hii ya kutalii kazi tangulizi, tutajikita katika kubainisha kiunzi cha nadharia ambayo tutaitumia tunapochunguza mofu njeo, aina zake na mazingira ya kutokea kwake. Kiunzi cha nadharia tutakayoizingatia ni nadharia ya ulalo ya Reichenbach.

2.4.1 Nadharia ya ulalo ya Reichenbach

Nadharia ya ulalo ya mahusiano ya nyakati katika lugha iliasisiwa na Reichenbach (1947) kushughulikia masuala ya nyakati katika lugha ya Kiingereza. Kwa mujibu wa nadharia hii nyakati katika lugha huelezwa kwa alama tatu muhimu: a) alama ya muda wa mazungumzo (amm), b) alama ya muda wa tukio (amt) na c) alama ya muda rejelewa (amr).

Reichenbach (ameshatajwa) alionyesha tofauti zilizopo katika mofu njeo za lugha ya Kiingereza kwa kuangalia uhusiano unaokuwepo kati ya alama hizi tatu za wakati. Ameeleza kuwa uhusiano wa alama hizi unaweza kuwa wa usambamba au wa kufuatana. Amefafanua kuwa, si lazima alama rejelewa iwe wakati uliopo unaobainishwa katika sentensi au usemi fulani bali alama rejelewa huweza kubainishwa kwa kuangalia muktadha katika kubainisha muda wa tukio. Kwa mujibu wa Reichenbach, njeo huweza kubainishwa kwa kuangalia matini nzima. Hivyo, ameonyesha kuwa mahusiano ya nyakati si lazima yatazamwe katika kiwango cha sentensi bali huweza kutazamwa kwa kuzingatia matini nzima. Kwa maelezo haya inaonyesha kuwa si kila mara muda rejelewa ni wakati uliopo bali unaweza kubainishwa kwa kuzingatia maarifa waliyonayo wazungumzaji.

Pili, nadharia hii inahusisha maumbo ya njeo na maumbo mengine ya kisarufi ambayo yangeweza kuainishwa kama dhamira au hali. Mfano wa dhamira ni: *ninaimb-a*, *imb-a*, *imb-eni*, *usiimb-e*. Mfano wa hali ni: *nimeimba*, *sijaimba*, *akanunua*, *akicheza*.

Smith (1978) aliboresha nadharia hii kwa kubadilisha alama rejelewa iliyopendekezwa na Reichenbach na kuwa muda rejelewa (mr) ambao ni muda mahususi wa tukio. Pia aliona ni vema kutumia neno tofauti za wakati badala ya alama za wakati pindi tunapozungumzia mahusiano ya nyakati katika lugha.

Wakati unaweza kuwasilishwa katika sentensi kwa kufuata uhusiano wa kigezo bainifu cha ukweli ambao huendana na ulimwengu kwa kufuata aina tatu za wakati ambazo ni: wakati uliopo, kipindi cha muda fulani/ kati ya muda fulani (muda rejelewa wa mazungumzo) na muda ujao (Johnson (1977)). Aidha, anaendelea kusema kuwa katika kutambulisha wakati mofu njeo ujitokeza katika njia tofauti kwa masharti ya kufasili sentensi ili ilete ukweli, unaofanya kazi ndani ya mfumo wa semantikia. Kwa hali hii, katika Kikuyu mofu njeo inajumuisha wakati uliopita: siku nyingi zilizopita, wakati uliopita (jana), mapema ndani ya siku ya mazungumzo. Wakati uliopo na wakati ujao: muda ujao saa chache baada ya muda wa mazungumzo na muda ujao mrefu kuanzia kesho na kuendelea.

González (2003) anakubaliana na nadharia hii ya Reichenbach, mofu njeo huonesha wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao. Katika utafiti huu, mtafiti hakushughulikia mofu hali bali mofu njeo, hivyo, hakuendelea na mofu hali ya kama alivyotafiti González.

Utafiti huu unatumia nadharia ya ulalo katika kuchambua mofu njeo katika lugha ya Kikara na Kiswahili ili kujua mahusiano ya nyakati. Hata hivyo, mtafiti atatumia tofauti za wakati kama alivyopendekeza Smith (ameshatajwa) badala ya alama za wakati zilizotumiwa na Reichenbach.

Kwa ujumla, nadharia hii imekuwa na manufaa sana katika utafiti huu kwa sababu inatuwezesha kuchunguza nafasi ya mofu njeo, kubaini tofauti ya idadi ya mofu njeo na mazingira yanayojitokeza baina ya lugha hizo mbili na hivyo kulinganisha mofu njeo za Kikara na za Kiswahili. Nadharia hii hudhihirisha upekee wa kila lugha na hutumika katika mofu njeo, tumechunguza lugha hizi mbili tukajua idadi, nafasi na mazingira mofu njeo zinapotokea.

2.5 Hitimisho

Sura hii ilipitia machapisho mbalimbali kuhusu mofu njeo ambayo yalitoa changamoto kwa mtafiti kuweza kufanya utafiti wa kiisimu kwa kulinganisha mofu za njeo za Kikara na za Kiswahili. Mapitio ya machapisho hayo yalionesha jinsi mofu njeo hutofautiana katika nafasi zinapotokea, idadi na mazingira zinapotokea. Sura inayofuata inaelezea mbinu za utafiti na nadharia ya utafiti iliyotumika. Nadharia na mbinu za utafiti zilisaidia katika uwasilishaji na uchambuzi wa data na kufikia hitimisho.

SURA YA TATU

3.0 USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza usanifu na mbinu za utafiti zilizotumika katika mchakato wa utafiti huu. Mbinu za utafiti zinajumuisha eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya data, aina ya data iliyokusanywa, zana za kukusanyia data na uchambuzi wa data.

3.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpango unaoonyesha jinsi utafiti utakavyofanywa katika kuchunguza tatizo la utafiti. Usanifu wa utafiti hueleza mbinu za utafiti zitakazotumiwa, namna data itakavyokusanywa, zana za utafiti za kukusanyia na uchambuzi wa data. Kothari (2004).

Usanifu wa utafiti huonyesha jinsi ambavyo vipengele mbalimbali vya utafiti hujumuishwa pamoja. Kwa hivyo usanifu wa utafiti ni utaratibu wa kuchunguza tatizo kisayansi. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006) usanifu wa utafiti ni mpangilio wa taratibu zinazotumika kukusanya na kuchambua data kwa namna inayounganisha data zinazopatikana na malengo ya utafiti.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika kata za Bukiko na Nyamanga, tarafa ya Ukara wilaya ya Ukerewe, mkoa wa Mwanza. Eneo hili lilitolewa kwa sababu lina wasomi wenye umri mkubwa ambao wanafahamu Kikara na Kiswahili vizuri. Pia kata hizi

zilizingatiwa kwa kuwa Nyamanga ni sehemu ya makao makuu ya Kanisa Katoliki (parokia) waliosoma semenari ni wengi na Bukiko ni sehemu ambayo mtemi alikuwa akiishi.

3.4 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti zimefafanuliwa na Kothari (2004) kuwa, ni jumla ya mbinu zinazotumiwa katika kukusanyia data. Mbinu za kukusanyia data ni mbinu zile ambazo mtafiti huzitumia ili kupata taarifa za utafiti. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu ya usaili, na utumiaji wa dodoso katika kukusanya data.

3.4.1 Usaili

Mbinu hii inahusisha uwasilishaji wa maswali kwa watafitiwa. Maswali hayo yatajibiwa kwa mdomo wakati huohuo mtafiti atarekodi majibu hayo katika tepu ya kurekodia au ataandika katika daftari la kumbukumbu. Kwa mujibu wa Kothari (2004) na Mligo (2012) mbinu hii inamruhusu mtafiti kuuliza maswali ya nyongeza. Hatimaye husaidia kuweka bayana jambo ambalo halieleweki kwa watu wanaoulizwa maswali. Hivyo basi, katika utafiti huu usaili ulitumika ili kupata data ya mofu njeo za Kikara. Pamoja na hayo, katika mbinu hii mtafiti alitumia zaidi usaili maalumu ambao watafitiwa waliulizwa maswali ya msingi ya aina moja na yaliyo katika mpangilio ulio sawa. Mtafiti aliandaa maswali ambayo yalilenga kukusanya taarifa za aina moja kwa kila kundi la watafitiwa.

3.4.2 Dodoso

Kwa mujibu wa Kothari (2004) na Mligo (2012) dodoso ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti anaandaa maswali yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo

fulani. Katika utafiti huu mtafiti aliwapa watafitiwa dodoso yenye lugha ya Kikara na Kiswahili wanaoifahamu na kuelewa vizuri kwa usahihi. Dodoso hizi ziliandikwa vitenzi peke yake katika lugha ya Kiswahili na sentensi za Kiswahili peke yake ili ziandikwe katika lugha ya Kikara na sentensi za Kikara ziliandikwa kwa Kiswahili. Kwa kutumia mbinu hii ilisaidia katika kulinganisha data za mofu za njeo za Kikara na za Kiswahili.

3.5 Aina ya Data Iliyokusanywa

Data hupatikana kutokana na vyanzo mbalimbali kama inavyoelezwa hapa. Kothari (2004) na Mligo (2012) wanakubaliana kuwa, zipo aina kuu mbili za data ambazo ni data ya msingi na data ya upili.

3.5.1 Data ya Msingi

Data ya msingi ilikusanywa uwandani wakati mtafiti alipowahoji watafitiwa kuhusu mofu njeo za Kikara. Data hii ilikusanywa na mtafiti moja kwa moja kutoka kwenye eneo la utafiti. Kwa mujibu wa Mligo (2012:104) na, Kombo na Tromp (2006:100) data ya msingi ni taarifa ambazo hukusanywa moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa Kothari (ameshatajwa:95) anafafanua zaidi kwa kusema kuwa data ya msingi ni data ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza, ni halisi, na hutokea kuwa asilia. Data ya msingi ilikusanywa uwandani kisiwani Ukara na mtafiti moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa ambao ndio wazungumzaji wa lugha hii kupitia mbinu za usaili na dodoso.

3.5.2 Data ya Upili

Data upili ni data ambazo tayari zimekusanywa na mtu mwingine na ambazo tayari

zimepitia mchakato wa kitakwimu Kothari (ameshatajwa: 95). Utafiti huu utatumia data ya msingi tu kwani hakuna data ya upili iliyopo ambayo mtafiti angeitumia.

3.6 Sampuli na Usampulishaji

3.6.1 Sampuli

Mlilo (2012:60) anasema sampuli ni kundi la watu ndani ya mkusanyiko mkubwa wenye uelewa unaofanana kuhusu tatizo analoshughulika nalo mtafiti. Kothari (2004) anasema kwamba sampuli humaanisha watu walioteuliwa kujibu maswali ya utafiti kutoka katika kundi husika. Uteuzi wa sampuli ni muhimu kwa sababu si rahisi kwa mtafiti kuwahoji watu wote wanaoishi eneo husika.

3.6.2 Usampulishaji

Ni mchakato wa kuchagua sampuli ya watoa habari kutoka katika kundi lengwa la utafiti. Katika mchakato huu mshiriki yeyote katika kundi lengwa anakuwa na fursa ya kuchaguliwa. Usampulishaji ni wa aina tatu: usampulishaji lengwa, usampulishaji makusudio na usampulishaji nasibu.

3.6.3 Usampulishaji Lengwa

Kwa mujibu wa Kothari (2004) kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika kazi ya utafiti. Walengwa waliohusishwa katika utafiti huu ni walimu, wazee, wasomi wa zamani wa shule za seminari na wananchi, kutoka katika kata hizo mbili za Bukiko na Nyamanga ambazo zipo katika tarafa ya Ukara wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza. Kundi hili watafitiwa katika utafiti huu lilitolewa

kulingana na sifa na umuhimu wa kila kundi. Katika utafiti huu, walimu ambao wana uzoefu na maarifa katika lugha kutoka kata hizo walihusishwa. Hivyo basi, utafiti huu uliliona kundi hilo kuwa ndilo lenye uwezo wa kutoa data sahihi juu ya mofu njeo za Kikara kwa kuandika vitenzi walivyopewa kwenye dodoso. Pia kigezo cha wasomi waliosoma seminari kilimfanya mtafiti kuliona kundi hili kuwa ni rasilimali ya kutosha katika utoaji wa data. Wazee na wananchi waliteuliwa kwa sababu wao wana umilisi wa lugha zote mbili.

3.6.4 Usampulishaji Nasibu

Kwa mujibu wa Kothari (2004) usampulishaji nasibu ni mbinu ya kuchagua sampuli ambayo kila mshiriki katika kundi ana fursa sawa ya kuchaguliwa. Kwa maneno mengine usampulishaji nasibu na usampulishaji lengwa ni mbinu ya kuchagua sampuli ambayo huegemea zaidi uamuzi wa mtafiti na hauwezi kutoa matokeo jumuisi kuhusiana na kundi lengwa. Hii ina maana kuwa, ni mbinu ya kuchagua sampuli ambayo sehemu ya watafitiwa huchaguliwa kwa kuzingatia zaidi upatikanaji wao kuliko uwakilishi wao.

3.6.5 Usampulishaji Makusudio

Hii ni mbinu ya kuchagua sampuli ambayo mtafiti huichagua huku akiwa na matarajio kuwa itawakilisha kundi lengwa.

Utafiti huu ulitumia usampulishaji usio nasibu kwa maana ya uteuzi wa kukusudia. Mtafiti aliamua kutumia aina hii ya sampuli katika utafiti wake kwa sababu aliamini kuwa kundi hili ndilo lenye uwezo wa kutoa taarifa sahihi katika kufikia malengo ya utafiti huu. Pia uteuzi wa sampuli kimaeneo ulizingatia maeneo ya kiutamaduni, na

kielimu katika tarafa ya Ukara. Maeneo haya yalichaguliwa kwa sababu ya wingi wa watu waliosoma shule.

Sampuli ya utafiti ilikuwa na watafitiwa 45 ambao watafitiwa 10 miongoni mwao walikuwa walimu wazawa waliofundishwa Katekisimu ya Kikatoliki katika lugha ya Kikara na ambao walikuwa walimu wa shule za msingi na sekondari. Hawa waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa. Sampuli lengwa iliteuliwa kwa sababu wao wanajua lugha zote mbili kwa ufasaha. Watafitiwa 15 walikuwa ni wazee waliojifunza Katekisimu kwa lugha ya Kikara na ambao bado wanahudhuria katika ibada zao katika kata ya Bukiko na Nyamanga ambao waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji nasibu. Watafitiwa 5 wenye umri kati ya miaka 60 hadi 69 waliosoma zamani katika shule za seminari waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa. Watafitiwa 15 walikuwa wananchi wanaozungumza Kikara na Kiswahili.

3.7 Uchambuzi wa Data

Baada ya kukamilika kwa mchakato wa ukusanyaji wa data, mtafiti alichambua data. Katika mchakato huu, data iliwasilishwa kwanza na halafu ilichambuliwa. Kothari (2004) anafafanua kuwa kuchambua data ni kitendo cha kuchanganua, kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Uchambuzi wa data ni hatua muhimu katika kutafuta majibu ya tatizo la utafiti. Kwa msingi huu uchambuzi wa data utaongozwa na mbinu ya uchambuzi wa kinaelezo katika kuchambua data za utafiti huu. Mbinu hii ya kiuchambuzi, huruhusu utolewaji wa maelezo ya kina juu ya data zilizokusanywa na mtafiti kwa namna ambayo iliweza kukidhi na kujibu maswali ya utafiti husika.

Inafaa ieleweke kwamba, mtafiti anapozungumza kuhusu mbinu ya kimaelezo ana maana kwamba alichambua data kwa kuzitolea ufafanuzi wa kimaelezo usiohusisha kanuni zozote za kitakwimu. Data zilizokusanywa zilipangwa vizuri katika makundi mbalimbali yanayofanana ili kurahisisha uchambuzi wa data. Uchambuzi wa data ulifanywa kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti

3.8 Ukusanyaji wa Data

Data zilikusanywa katika jamii ya Wakara wanaoishi katika Kata za Bukiko na Nyamanga. Kata hizi zilizingatiwa kwa kuwa Nyamanga ni sehemu ya makao makuu ya Kanisa Katoliki (parokia) na Bukiko ni sehemu ambayo mtemi alikuwa akiishi na sehemu zote hizi zina watu wengi na wasomi. Kwa sababu hii zilimsaidia mtafiti kukusanya data kwa urahisi. Ukusanyaji wa data za utafiti huu ulifanyika katika sehemu ndogo sana katika tarafa ya Ukara. Usaili wa ana kwa ana ulihusika wakati wa kukusanya data ya msingi. Hii ni kwa sababu baadhi ya data za kiutendaji haziwezi kupatikana bila kukutana na watafitiwa ambao ndio wenye kutoa data toshelevu na za kina zilizohitajika. Mtafiti aliwapa watoa habari dodoso zilizoandikwa vitenzi 9 vya Kiswahili, sentensi 15 za Kiswahili ili watafsiri katika Kikara na sentensi 11 za Kikara ili watafsiri katika Kiswahili. Watafitiwa walishiriki vizuri kwa kujaza dodoso walizopewa na mtafiti.

Mtafiti alinukuu kwenye daftari yale mambo yote muhimu yaliyomwezesha kufikia malengo ya utafiti.

3.9 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza mbinu mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji wa data na namna ya uwasilishaji na uchambuzi wa data. Mbinu hizo ndizo zilizoongoza uchakataji wa data na kuweza kukamilisha kazi hii ya utafiti. Mbinu zilizojadiliwa katika sura hii zilisaidia katika uwasilishaji na uchambuzi wa data kama tutakavyoona katika sura ya nne. Sura inayofuata inaeleza uwasilishaji wa data za mofu nje za Kikara na za Kiswahili.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA MOFU NJEO ZA

KIKARA NA ZA KISWAHILI

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kuchambua data zinazohusu mofu njeo za Kikara na za Kiswahili. Uwasilishaji na uchambuzi huu wa data umefanywa na kuongozwa na malengo na maswali ya utafiti. Data ziliwasilishwa kwa maelezo na kufafanuliwa kwa mifano ya mofu njeo husika. Katika mjadala huu tunawasilisha na kuchambua mofu njeo za Kikara na Kiswahili na kisha kuzilinganisha kwa mujibu wa malengo yetu ya utafiti. Kabla ya kuwasilisha data yafaa turejeele malengo ya utafiti huu ambayo ni:

- i) Kuchunguza nafasi ya mofu njeo katika kitenzi cha Kikara na cha Kiswahili ili kuona mazingira zinamotokea.
- ii) Kubaini idadi ya mofu njeo za Kikara na za Kiswahili ili kubaini iwapo ni sawa au la.
- iii) Kuonyesha mazingira ya mofu njeo na jinsi inavyoathiriwa na umbo la kitenzi ambamo mofu inatokea .
- iv) Kulinganisha mofu njeo za Kikara na Kiswahili ili kuona iwapo zinatokea katika nafasi ile ile au la.

4.2 Uwasilishaji wa Data

Katika uwasilishaji huu tutaanza kuangazia mofu njeo za Kikara na kisha mofu njeo za Kiswahili. Uwasilishaji na uchambuzi wa data utafanyika kwa kuzingatia lengo

kuu na malengo mahsusi ya utafiti wa mada hii pamoja na maswali ya utafiti yanayoambatana na hayo malengo. Tutaanza na lengo mahsusi la kwanza hadi la nne, halafu tutalinganisha mofu njeo za lugha hizi.

4.2.1 Nafasi ya Mofu Njeo Katika Kitenzi cha Kikara

Katika sura ya kwanza tulieleza kuwa mofu njeo ni umbo la kimofolojia ambalo hurejelea uhusiano kati ya muda wa mazungumzo na tukio katika lugha. Tulieleza pia kuwa mofu njeo katika lugha ni za aina tatu a) mofu njeo ya wakati uliopita, b) mofu njeo ya wakati uliopo, na c) mofu njeo ya wakati ujao.

Mofu njeo katika Kikara hutofautishwa katika wakati uliopita, uliopo na ujao. Mofu njeo katika Kikara hugawanyika katika makundi mawili ambayo hujitokeza katika uyakinifu na ukanushi. Lugha ya Kikara ina mofu njeo za aina tatu pia ambazo ni: a) mofu njeo ya wakati uliopita, b) mofu njeo ya wakati uliopo, na c) mofu njeo ya wakati ujao. Katika sehemu inayofuata tunawasilisha mofu njeo za Kikara za wakati uliopita.

4.2.1.1 Mofu Njeo ya Kikara Wakati Uliopita (Njeopita)

Mofu njeo ya wakati uliopita ya vitenzi vya Kikara ni: { *-ile* } na kabadala chake { *-ele* }, na { *-ma-* } na kabadala chake { *-me-* }. Uwepo wa mofu njeo mbili za wakati uliopita katika Kikara unamaanisha kuwa lugha hii ina viwango viwili vya wakati uliopita ambavyo huwakilishwa na mofu njeo (2) tofauti. Viwango hivi vya wakati uliopita ni: *wakati uliopita kitambo* na *wakati uliopita wa karibu* ambao kila moja huwakilishwa na mofu njeo mahsusi kwake, yaani mofu njeo wakati uliopita kitambo

na mofu njeo wakati uliopita wa karibu kwa mfuatano huo. Tuanze na mofu njeo wakati uliopita kitambo.

(i) *Mofu njeo wakati uliopita kitambo*

Wakati uliopita kitambo ni wakati unaoelezea matendo yaliyotendeka zaidi ya siku mbili kabla ya muda wa mazungumzo kama vile juma, mwezi, miezi na miaka iliyopita. Mofu njeo ya wakati uliopita kitambo katika vitenzi ina maumbo mawili: {-ile} na {-ele}

Mfano: 1

i) na- kam- *ile*

nfs1um -mzz-njeopita

‘nilikama’

ii) wa- sek- *ele*

nfs 2 um- mzz- njeopita

‘ulicheka’

iii) a- sing- *ile*

nfs 3 um- mzz- njeopita

‘alishinda’

iv) cha- mot- *ele*

nfs1wi- mzz- njeopita

‘tulifua’

v) mwa- suβ- *ile*

nfs 2 wi- mzz- njeopita

‘mlirudi’

Mofu njeo ya wakati uliopita kitambo kama data ya Mfano: 1 juu inavyoonyesha ni {-ile} na {-ele}. Kwa kuzingatia mazingira ya kutokea mofu hizi, ni dhahiri kuwa mofu {-ile} na {-ele} ni mofu moja yenye maumbo tofauti kwani zote hutokea katika mazingira yale yale ya kitenzi. Tofauti za maumbo haya zinatokana na umbo la irabu iliyo katika mzizi wa kitenzi husika. Mofu njeo {-ele} huambatana na kitenzi chenye irabu /e/ au /o/ katika mzizi wake, na mofu njeo {-ile} hufuatana na kitenzi chenye irabu /a/, /i/ au /u/ kwenye mzizi wake. Mofu {-ile} ina mawanda mapana zaidi kuliko mofu {-ele} kwa hivyo tunaibainisha kama umbo la msingi. Kwa hali hii, {-ile} ndiyo mofu na {-ele} ni alomofu ya {-ile}

(ii) *Mofu njeo ya wakati uliopita wa karibu*

Wakati uliopita wa karibu ni wakati unaoelezea matendo yaliyotendeka siku moja kabla ya siku ya mazungumzo kama vile jana. Mofu njeo ya wakati uliopita wa karibu katika vitenzi ina maumbo mawili: {-ma-} na {-me-}

Mfano: 2

i) na- ma- tay- a

nfs 1 um-njeopita- mzz- ir.mw

‘nilichota’

ii) cha- ma- tek- a

nfs 2 wi- njeopita- mzz- ir.mw

‘tulipika’

iii) wa- ma- liny- a

nfs 2 um- njeopita- mzz- ir.mw

‘ulipanda’

iv) mwa- *ma-* sol- a

nfs 2 wi- njeopita- mzz- ir.mw

‘mlichagua’

v) β a-*ma*-suk-a

nfs3 wi-njeopita- mzz-ir.mw

walimwaga’

vi) na- *ma-* nj- a

nfs1 um- njeopita- mzz-ir.mw

‘nilitandika’

vii) a- me- ny- a

nfs3 um-*njeopita*- mzz- ir.mw

‘a-li-chez-a’

viii) cha- *me-* t- a

nfs2 wi- njeopita- mzz- ir.mw

‘tuliua’

ix) β a- ma- ol- a

nfs 3 wi- njeopita- mzz- ir.mw

‘wa-li-pon-a’

x) na- *ma-* uul- a

nfs1 um- njeopita- mzz- ir.mw

‘ni-li-pur-a’

Mofu njeo ya wakati uliopita wa karibu kama ilivyoonyeshwa katika data ya Mfano:

2 juu ni: {-ma-} na {-me-}. Mofu njeo {-ma-} hutokea iwapo mzizi wa kitenzi unaanza na irabu /a/, / e/, / i /, /o/ au /u/: lakini mofu njeo hii {-ma-} hudondosha irabu /-a / ya kitenzi: ma+anj-a > ma-nja na mofu njeo {-me-} hutokea iwapo kitenzi kinaanza na irabu / e / au /i/ ambayo irabu hiyo inakuwa katika mzizi wa kitenzi.

Hii inatokana na mabadiliko ya kimofofolojia ambapo mofu {-ma-} yenye irabu /a/ inapofuatana na irabu /e / au /i / inayoanza katika kitenzi ambayo huungana na umbo la /e/ hutokea. Muungano huu ni wa irabu /a / ya mofu na irabu /e / au /i / inayoanza ya kitenzi hutokea mofu {-me-}.

Kwa kuwa mazingira ya kutokea mofu hizi yanafanana, ni hakika kuwa mofu {-ma-} na {-me-} ni mofu moja yenye maumbo tofauti kwa kuwa yanatokea katika mazingira yale yale. Tofauti za maumbo haya zinatokea iwapo kitenzi kinaanza na irabu / e / au / i / ambayo pia inakuwa katika mzizi wa kitenzi.

4.2.1.2 Nafasi ya Mofu Njeo Wakati Uliopita Katika Kitenzi

Mofu njeo za wakati uliopita zinatokea katika nafasi tofauti katika kitenzi. Mofu njeo ya wakati uliopita kitambo hutokea baada ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi tamati.

Mfano:3

- i) na- kam- *ile*
 nfs1um - mzz- njeopita
 nilikam-a'
- ii) wa- sek- *ele*

nfs 2 um- mzz- njeopita

ulicheka’

iii) a- suuk- *ile*

nfs 3 um- mzz- njeopita

‘alifufuka’

Katika mifano hii tunaona nafasi za mofu njeo {-*ile*} na {-*ele*} za wakati uliopita kitambo zinatokea baada ya mzizi wa kitenzi. Mofu njeo ya wakati uliopita karibu hutokea baada ya mofu nafsi na kabla ya mzizi wa kitenzi.

Mfano:4

i) wa- ma- liny- a

nfs 2 um- njeopita- mzz- ir.mw

‘ulipanda’

ii) mwa- ma- sol- a

nfs 2 wi-njeopita- mzz- ir.mw

‘mlichagua’

iii) a- me- ny- a

nfs 3 um-njeopita- mzz- ir.mw

‘alicheza’

iv) cha- me- t- a

nfs 2 wi- njeopita- mzz- ir.mw

‘tu-li-u-a’

Kutokana na mifano hii, mofu njeo ya wakati uliopita karibu ni kiambishi awali. Hii ni tofauti na mofu njeo wakati uliopita kitambo ambapo mofu njeo huwa kiambishi tamati.

4.2.2 Mofu njeo ya Kikara Wakati Uliopo (njeopo)

Wakati uliopo ni wakati ambapo tendo hutokea sambamba na muda wa mazungumzo. Kwa hivyo tukisema ‘*netaya*’ (ninachota) tunadokezwa kuwa tendo la kuchota linafanyika wakati ule ule mazungumzo kuhusu tukio hilo yanapofanyika. Mofu njeo ya wakati uliopo katika Kikara inawakilishwa na {-e-}

Mfano:5

i) n- e- tay- a

nfs1 um /- njeopo - mzz- ir.mw

‘ni-na-chot-a’

ii) w- e- sek-a

nfs 2 um /- njeopo - mzz-ir.mw

‘u-na-chek-a’

iii) β- e- liny- a

nfs 3 wi /- njeopo- mzz- ir.mw

‘wanapanda’

iv) ch- e- nok- a

nfs1wi /- njeopo - mzz- ir.mw

‘tunachuma’

v) mw- e- suβ-a

nfs2wi /- njeopo – mzz- ir.mw

‘mnarudi’

vi) e- ol- a

nfs 3 um/- njeopo - mzz-ir.mw

‘anapona’

vii)β- e – uul- a

nfs 3 wi - njeopo- mzz- ir.mw

‘wanapura’

Mofu njeo ya wakati uliopo {-e-} inatokea katika mazingira yote. Hii ni tofauti na mofu njeo za wakati uliopita ambazo umbo la mofu liliathiriwa na umbo la irabu katika mzizi wa kitenzi. Mofu njeo {-e-} ya wakati uliopo inapopakana na mofu nafsi yenye umbo la irabu, mathalani nafsi ya tatu umoja husababisha mofu nafsi /a-/ iungane na mofu njeo {-e-} ya wakati uliopo. Katika muungano huu irabu / a-/ hudondoshwa na mofu njeo {-e-} huchukua dhima ya mofu nafsi pia.

Mfano: 6

i) e- sek- a

nfs 3 um/-njeopo- mzz- ir.mw

‘anacheka’

ii) e- ol- a

nfs 3 um/-njeopo - mzz- ir.mw

‘anapona’

Iwapo mofu nafsi isingedondoshwa tungekuwa na kitenzi chenye umbo kama inavyoonyeshwa katika mfano wa 7 chini:

Mfano: 7

* *a- e- sek-a*
 nfs 3um-njeopo- mzz- ir.mw
 ‘anacheka’
 * *a- e- ol- a*
 nfs 3um-njeopo- mzz- ir.mw
 ‘anapona’

Wakati uliopo katika kitenzi ambacho mzizi wake huanza na irabu / i /, /e / na / a / kabla ya mzizi kuchopekwa kiambishi kisoukomo *-ku-* mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi. Kutokana na mfuatano wa irabu /u-/ ya kiambishi kisoukomo *-ku-* kati ya / i /, / e / na / a / hutokea mabadiliko yenye kuifanya *-ku-* kuwa *-kw-*. Hii inatokana na kusawazisha matamshi baina ya irabu juu / u / na nusu irabu / w /

Mfano:8

i) *n- e- anj- a*
 nfs1 um –njeopo- mzz- ir. Mw
n- e + ku + anj- a > n- e- kwanj- a
 nfs 1 um- njeopo- ks- mzz- ir. mw > nfs 1um- njeopo-mzz – ir.mw
 ‘ninatandika’
 ii) *w- e- eny-a*

nfs2 um - njeopo- mzz- ir.mw

w- e + ku + eny-a > w- e- kweny- a

nfs2 um-njeopo- ks- mzz- ir.mw > nfs 2 um –njeopo- mzz – ir.mw

‘unacheza’

iii) mw- e- it- a

nfs 2 wi -njeopo- mz- ir.mw

mw- e + ku+ it- a > mw- e- kwit- a

nfs2wi- njeopo- ks- mzz-ir. mw > nfs 2 wi - njeopo- mzz – ir.mw

‘m-na-u-a’

Iwapo irabu zinazokabiliana zisingebadilika umbo la kitenzi lingekuwa kama mfano huu unaoonyeshwa hapa chini:

Mfano: 9

i) n- e- anj- a

nfs 1 um -njeopo- mzz-ir.mw

‘ninatandika’

ii) w- e- eny- a

nfs 2 um-njeopo- mzz- ir.mw

‘unacheza’

iii) mw- e- it- a

nfs 2 wi -njeopo-mzz-ir.mw

‘mnaua’

Hali hii ya kukabiliana kwa irabu hutokea pia katika mofu kanushi ambapo {-ta-}

inakabiliana na mofu njeo {-e-} irabu /a-/ ya mofu kanushi {-ta-} hudondoshwa. Matokeo yake ni kwamba irabu / a / ya mofu kanushi hudondoka na kubaki konsonanti / t /. Konsonanti / t / inapokabiliana na mofu njeo {-e-} na kusahilisha matamshi kuwa {te-} ikiwa ni konsonanti / t /na mofu njeo {-e-}.

Mfano:10

- i) ni- t- e- tay- a
nfs1um- kan -njeopo- mzz- ir.mw
'sichoti'
- ii) m- t- e- suß- a
nfs 2 wi- kan -njeopo- mzz- ir.mw
'hamrudi'
- iii) ßa - t- e- sol- a
nfs 3 wi- kan- njeopo- mzz- ir.mw
'hawachagui'

4.2.2.1 Nafasi ya Mofu Njeo Wakati Uliopo Katika Kitenzi

Mofu njeo ya wakati uliopo hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali cha pili ambacho hufuata mofu nafsi ambayo ni kiambishi awali cha kwanza katika kitenzi yakinishi. Vile vile hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali cha tatu ambacho hufuata mofu kanushi ambacho ni kiambishi awali cha pili katika vitenzi kanushi.

Mfano: 11

- i) n- e- tay- a

nfs1 um /- njeopo - mzz- ir.mw

‘ninachota’

ii) w- e- sek- a

nfs 2 um/ -njeopo- mzz- ir.mw

‘unacheka’

iii) β- e- ku- anj- a (kwanj-a)

nfs 3 wi- njeopo - ks- mzz- ir.mw

‘wanatandika’

iv) u- t- e- ku- eny- a (kwenya)

nfs 2 um-kan-njeopo- ks- mzz- ir.mw

‘hu-chez-i’

v) chi- t- e- ku-ik- a

nfs 1 wi -kan -njeopo-ks- mzz- ir.mw

‘hatushuki’

Katika mifano hii tunaona mofu njeo {-e-} ikitokea kabla ya mizizi wa kitenzi k.v. {-tay-} ambao ni mzizi wa kitenzi ‘taya’ na mzizi {-sek-} wa kitenzi ‘seka’. Katika vitenzi vinavyoanza na irabu /a/, /e / na / i / huchopekwa kiambishi kisoukomo -ku- mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi kinachoanza na irabu / i /, /e / na / a / kutokana na mfuatano wa irabu kati ya mojawapo tunapata {-kw-} inayotokea kabla ya mzizi wa kitenzi.

Mfano: 12

i) n- e- anj- a

nfs1 um -njeopo- mzz- ir.mw

n-e + ku + anj-a > n-e-kwanj-a

nfs 1 um-njeopo-ks-mzz-ir.mw > nfs 1um- njeopo-mzz –ir.mw

‘ninatandika’

ii) w- e- eny- a

nfs2um - njeopo- mzz- ir.mw

w- e + ku + eny-a > w- e- kweny- a

nfs2um - njeopo- ks- mzz- ir.mw > nfs 2um - njeopo- mzz – ir.mw

‘unacheza’

iii) mw- e- ik- a

nfs 2 wi -njeopo- mzz- ir.mw

mw- e + ku+ it- a > mw- e- kwit-a

nfs2wi - njeopo- ks- mzz- ir.mw > nfs 2wi - njeopo-mzz – ir.mw

‘ninaua’

Katika wakati uliopo, kitenzi cha lugha ya Kikara kinachoanza na irabu / i /, /e / au / a / kwenye mzizi wa kitenzi hicho, huchopekwa *ku-* mwanzoni mwa kitenzi. Irabu /u / ya “ku-” inakutanishwa na irabu / i /, /e / au / a / ya mwanzo hubadilika kuwa nusu irabu / w /. Kutokana na mabadiliko haya, tunapata { - *kw-* } ambayo hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama mfano wetu 12 (i) mzizi { -anj- } hubadilika kuwa { -*kwanj-* }, (ii) mzizi { -*ik-* } hubadilika kuwa { -*kwik-* } na (iii) mzizi { -*eny-* } hubadilika kuwa { -*kweny-* }.

4.2.3 Mofu Njeo ya Kikara Wakati Ujao (Njeojao)

Wakati ujao ni wakati ambao hueleza tendo ambalo litafanyika au halitafanyika katika wakati ujao. Kikara kina viwango vitatu vya wakati ujao ambavyo ni: *wakati ujao kitambo*, *wakati ujao kitambo kiasi*, na *wakati ujao wa karibu*. Kila wakati unawakilishwa na mofu njeo mahsusi.

(i) Mofu njeo ya wakati ujao kitambo

Wakati ujao kitambo ni wakati unaoelezea matukio yatakayotokea kuanzia miaka miwili na zaidi baada ya muda wa mazungumzo. Mofu njeo katika kitenzi cha wakati ujao kitambo ni: *-li-*.

Mfano: 13

- i) a- *li-* eny- a
nfs3 um- njeojao- mzz- ir.mw
‘atacheza’
- ii) chi- *li-* βum-a
nfs1 wi- njeojao- mzz- ir.mw
‘tutapiga’
- iii) u- *li-* ol- a
nfs 2 um-njeojao- mzz-ir.mw
‘utapona’

Mofu njeo ya wakati ujao kitambo kama data ya Mfano 13 juu inavyoonyesha ni {*-li-*}. Mofu njeo wakati ujao kitambo inapofuatana na mofu nafsi yenye umbo la irabu au konsonanti hakuna athari yoyote inayotokea.

(ii) *Mofu njeo wakati ujao kitambo kiasi*

Wakati ujao kitambo kiasi ni wakati unaoelezea matukio yatakayotokea kuanzia siku mbili hadi mwaka mmoja baada ya muda wa mazungumzo.

Mofu njeo ya wakati ujao kitambo kiasi ni: {-ka- / -ke-} kwa kitenzi yakinishi na {-ku-/-kw-} kwa kitenzi kanushi.

Mofu njeo katika vitenzi yakinishi ni: {-ka-/-ke-}

Mfano: 14

i) βa- ka- tay-e
nfs 3-wi – njeojao - mzz- ir.mw

‘watachota’

ii) ii) cha- ka- kes- e
nfs 1 wi- njeojao- mzz- ir.mw

tutavuna’

iii) na- ka- liny- e
nfs 1 um -njeojao - mzz- ir.mw

‘nitapanda’

iv) wa- ka- sol- e
nfs 2 um-njeojao-mzz- ir.mw

‘utachagua’

v) mwa- ka- suβ- e
nfs 2 wi - njeojao – mzz-ir.mw

‘mtarudi’

vi) βa- ka- nj- e
 nfs 3-wi – njeojao - mzz-ir.mw
 ‘watatandika’

vii) a- ka- ol- e
 nfs 3 um -njeojao - mzz-ir.mw
 ‘ata pona’

viii) a- ka- um- e
 nfs3um-njeojao-mzz- ir.mw
 ‘atahama’

ix) na- k- eny-e
 nfs 1um-njeojao-mzz- ir.mw
 ‘nitacheza’

x) wa- k- ek- e
 nfs 2um-njeojao-mzz-ir.mw
 ‘utashuka’

xi) a- ke- t- e
 nfs3um-njeojao-mzz- ir.mw
 ‘ataua’

xii) βa- ke- timb-e
 nfs3um- njeojao-mzz- ir.mw
 ‘watasimama’

Mofu njeo {-ka-} hutokea katika kitenzi ambacho mzizi wake una irabu /a /, /e/, /i/, /o/ au /u/ pia kitenzi kinachoanza na irabu /a /, /o/ au /u/ kama katika mfano 14 vi), vii) na viii) hapo juu.

Mofu njeo {-ka-} inakuwa {-ke-} iwapo kitenzi kinaanza na irabu / e / au / i / kinapofuatana na irabu /-a / ya mofu njeo {-ka-}. Hii irabu /-a / ya mofu njeo hudondoshwa ikikabiliana na irabu / e / iliyo mwanzoni mwa kitenzi. Tazama, ix) “*enya*” inakuwa “*nakenye*”, lakini irabu / -a / ya mofu njeo {-ka-} inapofuatana na irabu / i / ambayo ipo mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi huvutana au huungana kwa kuwa zimetokea mahali pamoja taz, mfano 14 (x, xi na xii). Irabu chini /a/ inapokabiliana na irabu juu /i/ huathiriana na kuwa irabu kati /e/ na kuifanya mofu njeo {-ka-} katika mazingira haya kuwa {-ke-} kama katika Mfano: 14 (x, xi na xii).

Jedwali 4.1: Kusawazisha Matamshi Baina ya Irabu /a/ na / i / huzua irabu / e /

i
e
a

Turejee kwenye ufafanuzi hapa chini kutokana na mfano 14(ix, x, xi na xii) ambao tutauita Mfano:15.

Mfano 15

- i) na- *ka* +eny-a > na-*ke*-ny-e
- ii) wa-*ka* +ik-a > wa-*ke*-k-e
- iii) a-ka+it-a > a- *ke*-t-e
- iv) βa-ka+itimb-a > βa -*ke*-timb-e

Mazingira ya utokeaji wa mofu hizi ni yale yale, kwa hivyo ni dhahiri kuwa mofu {-ka-} na {-ke-} ni mofu moja yenye maumbo tofauti .Hii ni kwa sababu zote hutokea

katika mazingira mambo ya kitenzi. Tofauti za maumbo haya zinatokana na irabu /e / au /i/ iliyo mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi husika. Hii inaleta kuathiriana kunakosababishwa na irabu. Kwa hali hiyo huwa pia ni sehemu ya mofu njeo. Hii ni kwa sababu mofu njeo

{-ka-} haiendani na irabu ya mwisho –a ndiyo maana inaoneka {-ka-...-e} au {-ke-...-e}.

Mofu njeo ya wakati ujao kitambo kiasi katika vitenzi kanushi ni: {-ku-/-kw-}

Mofu njeo –ku- yakinishi na inavyotokea kuwa –kw- katika ukanushi. Taz. mifano ifuatayo:

Mfano: 16

i) a- ta- ku- tay- a

nfs3 um-kan-njeojao-mzz- ir.mw

‘hatachota’

ii) u- ta- ku- sek- a

nfs 2 um - kan-njeojao-mzz- ir.mw

‘hutacheke’

iii) βa- ta- ku- liny-a

nfs 3wi - kan- njeojao- mzz- ir.mw

‘hawata panda’

iv) chi- ta- ku- nok-a

nfs1wi-kan-njeojao-mzz- ir.mw

‘hatutachuma’

v) u- ta- ku- gulush-a

nfs 2 um-kan-njeojao- mzz- ir.mw

‘hutapepeta’

vi) βa- ta- kw- anj-a

nfs 3wi -kan- njeojao-mzz-ir-mw

‘hawatatandika’

vii) u- ta- kw- eny-a

nfs2 um- kan- njeojao- mzz-ir.mw

‘hutacheza’

viii) chi- ta- kw- ik-a

nfs2 wi- kan-njeojao- mzz-ir.mw

‘hatutashuka’

ix) a- ta- ku- ol-a

nfs 3 um-kan-njeojao - mzz-ir.mw

‘hatapona’

x) m- ta- ku- uul-a

nfs2 wi -kan-njeojao- mzz-ir.mw

‘hamtapura’

Mofu njeo ya wakati ujao kitambo kiasi ni{-ku-}. Mofu njeo hii inatokea baada ya mofu kanushi na kabla ya mzizi wa kitenzi, kama Mfano: 16 unavyoeleza hapo juu. Mofu njeo {-ku-} inakuwa {-ku-} iwapo mzizi wa kitenzi unakuwa na irabu /a/, /e /,

/i /, /o/ au / u / kama katika 16 i) hadi v). Hapa kuna mofu njeo moja tu yaani {-ku-} ambayo hubadilika na kuwa {-kw-} kutokana na mazingira ya kutokea kwake.

Tunaona kuwa, iwapo kitenzi huanza na irabu /o/ au /u/ kama katika 16 ix) na x) na ikiwa kitenzi kinaanza na konsonanti kama katika 16 i) hadi v) inaendelea kuwa {-ku-} lakini mofu njeo {-ku-} inakuwa {-kw-} iwapo kitenzi huanza na irabu /a/, /e/ au /i/ kama katika 16 vii) hadi viii).

Mofu njeo hii inatokea baada ya mofu kanushi na kabla ya mzizi wa kitenzi katika vitenzi kanushi, kama Mfano: 16 unavyoonyesha hapo juu. Mofu njeo {-ku-} inakuwa {-ku-} iwapo mzizi wa kitenzi unakuwa na irabu / a /, / e /, / i /, / o / au / u / lakini hubadilika na kuwa {-kw-} iwapo hufuatwa na kitenzi chenye mzizi unaanza na irabu / a /, / e / au / i /. Hii ni kwa sababu irabu /u/ ya mofu / ku / hubadilika na kuwa nusu irabu /w/ inapofuatana na irabu /a/, /e/ au /i / kama ilivyo katika Mfano 17.

Mfano: 17

i) β a- ta- ku- anj- a (β a-ta-kw-anj-a)

nfs 3wi- kan-njeojao-mzz-ir.mw

ii) u- ta- ku- eny-a (u-ta-kw-eny-a)

nfs 2 um -kan-njeojao- mzz-ir.mw

Mofu kanushi ku- yenye irabu / u- / ikifuatwa na irabu / a-/, / e-/, / i-/ au / o-/ hubadilika na kuwa nusuirabu / -w /. Kwa hiyo, tunasema kuwa irabu inapanda kutoka kwenye irabu na kuwa nusuirabu, kwa hali hiyo irabu imeimarika. Tazama

mifano yenye irabu / a- / ya kitenzi *anja* katika 17 i) na kuwa *kw-anja* na katika ii) *ku* inafuatwa na irabu / e-/ ya kitenzi *enye* na kuwa *kw-enya*. Kwa kuwa mazingira ya utokeaji wa mofu hizi katika kitenzi ni yale yale, ni dhahiri kuwa mofu {-ku-} na {-kw-} ni mofu moja yenye maumbo tofauti ambapo umbo moja ni mofu na jingine ni alomofu.

(iii) *Mofu njeo ya wakati ujao wa karibu*

Wakati ujao wa karibu ni wakati unaoelezea matukio yatakayotendeka au kutotendeka muda mfupi baada ya mazungumzo hadi masaa machache yajayo kabla ya siku inayofuata.

Mofu njeo wakati ujao wa karibu ni -ndo-

Mfano: 18

i) che- ndo- kes-a

nfs 1wi- njeojao- mzz-ir.mw

‘tutavuna’

ii) we- ndo- sol- a

nfs2 um- njeojao- mzz- ir.mw

‘utachagua’

iii) mwe- ndo- ku + anj-a > kwanja

nfs 2 wi -njeojao- ks- mzz-ir.mw

‘mtatandika’

iv) e- ndo- um-a

nfs 3um njeojao- mzz-ir.mw

‘a-ta-ha-m-a’

v) βe- ndo- ku + itimb-a > kwitimba

nfs 3wi- njeojao- ks- mzz- ir.mw

‘watasimama’

vi) ne- ndo- ku + eny-a > kwenya

nfs 1um-njeojao-ks- mzz-ir.mw

‘watasimama’

Mofu njeo wakati ujao wa karibu ni {-ndo-} kama Mfano: 18 hapo juu unavyoonesha. Irabu ya mofu nafsi /-a / inapofuatana na nazali /n/ iliyo katika mofu njeo {-ndo-} irabu /a/ inabadilika na kuwa /e/ katika mofu nafsi.

4.2.3.1 Nafasi ya Mofu Njeo Wakati Ujao Katika Kitenzi

Mofu njeo ya wakati ujao hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali cha pili kikifuata mofu nafsi ambayo ni kiambishi awali cha kwanza katika kitenzi.

Mfano: 19

i) a- li- eny-a

nfs3 um-njeojao- mzz- ir.mw

‘atacheza’

ii) chi- li- βum-a

nfs 1wi- njeojao- mzz- ir.mw

‘tutapiga’

iii) a- ka- βum-e

nfs3 um-njeojao- mzz- ir.mw

‘*atapiga*’

iv) cha- ka- um-e

nfs 2 wi-njeojao- mzz-ir.mw

‘*tutahama*’

v) β a- ke- s- e

nfs3wi-njeojao- mzz-ir.mw

‘*watatupa*’

Vile vile mofu njeo ya wakati ujao hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali cha tatu ambacho hufuata mofu kanushi ambacho ni kiambishi awali cha pili katika vitenzi.

Mfano:20

i) β a - ta- ku- β um-a

nfs 3 wi- kan- njeojao- mzz-ir.mw

‘*hawatapiga*’

ii) β a - ta- ku- um- a

nfs 3wi -kan- njeojao- mzz-ir.mw

‘*hawatahama*’

iii) β a- ta- kw- es-a

nfs 3wi-kan- njeojao- mzz-ir.mw

‘*hawatatupa*’

iv) β e- ndo- senj-a

nfs 3 wi-njeojao- mzz- ir.mw

‘watapalilia’

v) che- ndo- kwik-a

nfs2wi-njeojao- mzz- ir.mw

‘tutashuka’

Kutokana na mifano hii, mofu njeo ya wakati ujao kitambo, ujao kitambo kiasi na ujao wa karibu huwa pia kati ya mzizi na mofu nafsi na kati ya mzizi na mofu kanushi.

4.2.3.2 Idadi ya Mofu Njeo za Kitenzi cha Kikara

Kikara kina mofu njeo za kitenzi saba kama ifuatavyo:

1. *Mofu njeo wakati uliopita*

Wakati uliopita katika Kikara mofu njeo zipo za aina mbili ambazo ni:

(i) *Mofu njeo wakati uliopita kitambo*

Wakati uliopita kitambo una mofu njeo moja ambayo ni {*-ile*} na nyingine ni alomofu ambayo ni {*-ele*}

Mfano: 21

i) na-kam-*ile*

‘nilikama’

ii) wa-sek-*ele*

‘ulicheka’

iii) βa-ol-*ele*

‘walipona’

ii) Mofu njeo *wakati uliopita wa karibu*:

Wakati uliopita wa karibu una mofu njeo moja {-ma-} na alomofu {-me-}

Mfano:22

i) na-ma-kama

‘*nilikama*’

ii) a-me-nya

‘*alicheza*’

iii) cha-me-ka

‘*tulishuka*’

2. Mofu njeo ya wakati uliopo

Wakati uliopo una mofu njeo moja {- e-} inayojitokeza katika kitenzi.

Mfano: 23

i) n-e-tay-a

‘*ninachota*’

ii) w-e-kwes-a

‘*unatupa*’

3. Mofu njeo ya wakati ujao

Mofu njeo ya wakati ujao zipo nne kama zilizyoainishwa hapa chini:

i) Mofu njeo wakati ujao kitambo

Wakati ujao kitambo una mofu njeo moja {-li-} inayojitokeza katika kitenzi.

Mfano: 24

i) a-li-um-a

‘atahama’

ii) ni-*li*-laβ-a

‘nitaonja’

iii) βa-*li*-sing-a

‘watashinda’

ii) *Mofu njeo wakati ujao kitambo kiasi*

Wakati ujao kitambo kiasi una mofu njeo mbili: {-ka- /-ke-} na {-ku- / kw-}.

Mofu njeo {-ka-, -ke-} inajidhihirisha katika vitenzi vya Kikara kama ifuatavyo:

Mfano: 25

i) cha-*ka*-kes-e

‘tutavuna’

ii) βa-*ke*-timb-e

‘watasimama’

Mofu {-ku- /-kw-} inajidhihirisha katika vitenzi vya Kikara kama ifuatavyo:

Mfano: 26

i) chi-ta-*ku*-laβ-a

‘hatutaonja’

ii) βa-ta-*kw*-ik-a

‘hawatashuka’

iii) *Mofu njeo ya wakati ujao wa karibu*

Wakati ujao wa karibu una mofu njeo moja {-ndo-} inayojitokeza katika kitenzi.

Mfano: 27

- i) e-*ndo*-um-a
‘atahama’
- ii) ne-*ndo*-laβ-a
‘nitaonja’
- iii) βe-*ndo*-sing-a
‘watahinda’

4.2.4 Mazingira ya Mofu Njeo na Jinsi Inavyoathiriwa na Umbo la Kitenzi cha Kikara

Maumbo ya mofu njeo za vitenzi vya Kikara huathiriwa na mazingira ya mofu katika vitenzi zinamokuwa. Kama tulivyoeleza katika 4.2.1 juu, umbo la mofu huathiriwa na umbo la irabu ya mzizi wa kitenzi ambamo mofu njeo imeambatanishwa. Kwa mfano, mofu njeo {-*ile*} hufuatana na kitenzi chenye irabu / *a* /, /*i* / *au* / *u* / kwenye mzizi wake.

Mfano: 28

- i) na- kam-*ile*
nfs1um- mzz – njeopita
‘nilikama’
- ii) na- sing-*ile*
nfs1um- mzz- njeopita
‘nilishinda’
- iii) a- suuk- *ile*
nfs 3um- mzz- njeopita

‘alifufuka’

Mofu njeo {-ele-} huambatana na kitenzi chenye irabu /e/ au /o/ katika mzizi wake.

Mfano: 29

- i) i) wa- sek- *ele*
nfs 2 um-mzz- njeopita
‘ulicheka’
- ii) ii) ßa- sol-*ele*
nfs 3 wi-mzz-njeopita
‘alichagua’

Katika mfano wa 28 na 29 tunaona kwamba umbo la irabu katika mzizi wa kitenzi husababisha mofu njeo iwe {-ile }pale mzizi wa kitenzi unapokuwa na irabu / i /, / u / au / a / na inakuwa {-ele}pale mzizi wa kitenzi unapokuwa na irabu / e / au /o /.

Vivyo hivyo kwa, mofu njeo {-ma-} na alomofu yake {-me-}. Mofu njeo {-ma-} huambatana na kitenzi chenye mzizi wenye irabu /a /, /e/, /i/, /o/ au /u/

Mfano: 30

- i) na- ma- tay-a
nfs1um- njeopita -mzz- ir.mw
‘nilichota’
- ii) wa- ma- tek-a
nfs2 um -njeopita-mzz–ir.mw
‘ulipika’
- iii) cha- ma- sing- a

nfs 1wi-njeopita-mzz- ir.mw

‘*tulishinda*’

iv) mwa- *ma-* sol-a

nfs2 wi -njeopita-mzz -ir.mw

‘*mlichagua*’

v) a- *ma-* ol- a

nfs 3 um- njeopita- mzz -ir.mw

‘*alipona*’

vi) na- *ma-* uul- a

nfs 1um-njeopita- mzz-ir.mw

‘*nilipura*’

Mofu njeo{-*me-*}huambatana na kitenzi ambacho mzizi wake huanza na irabu /e / au /i /.

Mfano: 31

i) a- *me-* ny- a

nfs3 um-njeopita-mzz- ir. Mw

‘*alicheza*’

ii) cha- *me-* t- a

nfs 2wi- njeopita- mzz- ir. mw

‘*tulua*’

Tunaona kuwa umbo la irabu katika mzizi wa kitenzi ikiwa una irabu / a /, / e/ /i /, / o / au / u / husababisha iwe mofu njeo {-*ma-*} na inakuwa {-*me-*} pale kitenzi kinapoanza na irabu / e / au / i/.

Mabadiliko haya yanatokea pale ambapo irabu /e/ au /i/ inapofuata irabu /a/ ya mofu njeo {-ma-} ambayo ama haibadiliki na kubakia {-ma-} au /a/ hubadilika na kuwa /e/ na kuifanya mofu njeo {-ma-} kuwa {-me-}.

Mfano: 32

- i) na-ma-+ anja > na- ma-nja
- ii) a-ma-+enya > a-me-nya,
- iii) cha-ma+ ita > cha-me-ta
- iv) cha - ma + ota > cha-ma-ota
- v) βa-ma-+uula > βa-ma-uula

Katika mfano 32 i)-ii) tunaona kuwa irabu / a / ya mofu njeo {-ma-} imedondoshwa kwa kuwa imefuatana na irabu / a / au / e / iliyo mwanzoni mwa kitenzi.

Katika 32 iii) irabu / a / iliyo mwishoni mwa mofu njeo {-ma-} huungana au huvutana na irabu / i / iliyo mwanzoni mwa kitenzi 'ita' na hutokea irabu nyingine tofauti na zilizopo ambayo ni irabu /e / ilhali 32 v)-vi) mofu njeo {-ma-} inapofuatana na irabu /o / au / u / hakuna mabadiliko yanayotokea katika irabu au kitenzi.

Katika 4.2.2 tuliona umbo la / a / ya mofu nafsi inafuatiwa na mofu njeo {-e-}. Hapa /a / huathiriwa na umbo la mofu njeo {-e-} ambapo / a / inadondoshwa na mofu njeo / e / inabaki. Mfano, *na-e-tay-a* (ninachota) inakuwa (n-e-tay-a) “*netaya*” na / a / ya

ukanushi inafuatiwa na mofu njeo {-e-}. Hapa / a / huathiriwa na umbo la mofu njeo {-e-} ambapo / a / inadondoshwa na / e / inabaki. Mfano, *ni-ta-e-tay-a* (sichoti) inakuwa (ni-t-e-tay-a) “*nitetaya*”. Kwa hiyo, mabadiliko ya irabu / a / ya mofu nafsi na mofu ya ukanushi yanafanyika pale mofu njeo {-e-} inapokabiliana nazo na hutokea maathiriano.

Mfano: 33

- i) n- e- tay- a
nfs1 um /- njeopo - mzz- ir.mw
'ni-na-chot-a'
- ii) w- e- sek-a
nfs 2 um/ -njeopo- mzz-ir.mw
'unacheka'
- iii) u- t- e- tay- a
nfs 2 um -kan-njeopo- mzz- ir.mw
'hu-chot-i'
- iv) chi- t- e- sek-a
nfs 1 wi -kan -njeopo- mzz-ir.mw
'ha-tu-chek-i'

Mabadiliko ya kimofofonolojia hutokea katika kitenzi kinachoanza na irabu / i /, / e / au / a /. Katika mabadiliko haya *ku-* huchopekwa kati ya irabu iliyo mwanzoni mwa kitenzi na mzizi wa kitenzi baada ya mofu njeo. Mabadiliko haya hutokea baada ya irabu ya mofu nafsi kudondoshwa na kukabiliana na mofu njeo ambayo hufuatiwa na

kiambishi sioukomo *-ku-* ambacho kina irabu / u / ikikutanishwa na irabu / i /, / e / au /a / iliyo mwanzoni mwa kitenzi katika muunganiko huu hutokea nusu irabu / w / inayoambatana na konsonanti / k / ili kusawazisha matamshi tunapata {kw-} inayokuwa kwenye mzizi wa kitenzi kama Mfano 33 unavyoonesha hapa chini.

Mfano: 34

i) na- e- ku- eny-a > n-e-kw-eny-a

nfs1 um-njeopo-ks- mzz- ir.mw

‘ninacheza’

ii) cha- e- ku- it- a > ch-e-kw-it-a

nfs2 wi-njeopo- ks- mzz-ir.mw

‘tunaua’

iii))βa- e- ku- anj-a > β-e-kw-anj-a

nfs3 wi-njeopo- ks- mzz-ir.mw

‘wanatandika’

Vitenzi vinavyoanza na irabu /a/, /e / na / i / katika wakati uliopo huchopekwa *-ku-* mwanzoni mwa kitenzi.

Mfano: 35

i) we + e + ku- eny-a > w-e- kw-eny-a

nfs2 um- njeojao- ks- mzz-ir.mw

‘u-na-chez-a’

ii) cha + e + ku- it- a > ch-e-kw-it-a

nfs2 wi-njeopo- ks- mzz-ir.mw

tunaua’

Kwa hiyo, mabadiliko haya hutokea iwapo irabu ya mofu nafsi imedondoshwa na irabu ya mofu njeo imeungana na irabu ya mzizi wa kitenzi ambayo yaweza kuwa ama ni /i /, /e/ au /a/. Aidha, / u / ya `ku` inapofuatana na irabu /a /, /e / au / i / iliyo mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi, inakuwa nusu irabu /w/. Hii ina maana kuwa {ku} > {kw} iwapo {ku} inafuatwa na irabu /a/, /e/ au /i/ ambazo hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi.

Katika 4.2.3 tulieleza jinsi maumbo ya mofu njeo za vitenzi vya Kikara yanavyoathiriwa na mazingira yanayoambatana nayo. Mofu njeo {-ka-} huathiriwa na umbo la irabu ya mzizi wa kitenzi ambamo mofu njeo inaambatanishwa na kitenzi chenye irabu /u/, /o / au /a/ kwenye mzizi wake.

Mfano: 36

- i) na- k- anj- e
nfs1 um- njeojao – mzz -ir.mw
'nitatandika'
- ii) na- k- eny- e
nfs 1um- njeojao- mzz- ir.mw
'nitacheza'
- iii) βa- ke- timb-e
nfs3 wi- njeojao- mzz- ir.mw
'watasimama'

Mabadiliko haya hutokea pale ambapo mofu njeo {-ka-} yenye irabu / a / inapokutana na irabu / i /, / e / au / a / iliyo mwanzoni mwa kitenzi. Turejee kwenye

ufafanuzi hapa chini kutokana na mfano 36 (i, ii na iii) ambao tutauita Mfano: 37.

Mfano 37

- i) wa-*ka*-anj-a > wa-*k*-anj-e.
- ii) cha-*ka*-eny-a > cha-*ke*-ny-e.
- iii) β a-*ka*-itimb-a > β a-*ke*-timb-e

Hapa kinachotokea ni kuwa irabu /a / ya mofu njeo {-*ka*-} inakutana na irabu / a / inayoanza katika kitenzi. Irabu /a / ya mofu njeo {-*ka*-} hudondoshwa na kubakia irabu /a/ ya kwenye kitenzi kama katika Mfano 37 (i). Halikadhalika katika Mfano: 37 (ii) kinachotokea ni kuwa irabu /a / ya mofu njeo {-*ka*-} hukabiliana na irabu / e / inayoanza katika kitenzi, hivyo, mofu njeo hudondoshwa na kubakia irabu / e / ya kwenye kitenzi. Katika 37 (iii) irabu /a / ya mofu njeo na irabu / i / inayoanza katika kitenzi zikikutanishwa katika kingo za mipaka yake hubadilika na kuwa / e /. Kwa hiyo, tunaona mabadiliko ya mofu njeo {-*ka*-} hubadilika na matokeo tunapata mofu njeo {-*ke*-}. Kwa maana hii umbo la irabu katika mzizi wa kitenzi huathiri umbo la mofu njeo {-*ka*-} na kuifanya mofu iwe {-*ke*-}.

Mofu njeo {-*ku*-} huathiriwa na umbo la mzizi wa kitenzi ambamo mofu njeo inaambatanishwa na kitenzi chenye irabu /a /, /e /, /i /, /o/ au /u / katika mzizi wa kitenzi. Pia tulieleza kuwa mofu njeo {-*ku*-} ina kuwa {-*kw*-} katika mofu kanushi inapofuatana na irabu /a /, /e/ au /i / ambayo huanza mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi. Hii inaonyesha jinsi inavyoathiriwa na umbo la kitenzi ambamo mofu inatokea.

Mfano: 38

i) $\beta a + ta + ku - anj - a > \beta a - ta - kw - anj - a$

nfs 3wi- kan- njeojao- mzz-ir.mw

‘hawatatandika’

ii) $u + ta + ku - eny - a > u - ta - kw - enya$

nfs2 um- kan- njeojao- mzz-ir. mw

‘hutacheza’

iii) $chi + ta + ku - ik - a > chi - ta - kw - ik - a$

nfs 1 wi-kan-njeojao- mzz- ir.mw

hatutashuka’

4.3 Nafasi ya Mofu Njeo Katika Kitenzi cha Kiswahili

Mofu njeo za lugha ya Kiswahili huwakilisha nyakati kuu tatu: wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao.

4.3.1 Mofu Njeo za Wakati Uliopita

Mofu njeo wakati uliopita katika Kiswahili unaelezea tendo lililotendeka au ambalo halikutendeka kabla ya kutolewa kwa taarifa.

Mofu njeo katika vitenzi vya Kiswahili kwa wakati uliopita ni mbili: {-li-} kwa kitenzi yakinishi na {-ku-} kwa kitenzi kanushi.

Mofu njeo {-li-}

Mfano: 39

i) $ni - li - andik - a$

nfs1um- njeopita- mzz- ir.mw

- ii) tu- *li*- chum- a
 nfs 1wi- njeopita- mzz- ir.mw
- iii) u- *li*- chez- a
 nfs 2um- njeopita- mzz- ir.mw
- iv) m- *li*- ib- a
 nfs 2wi- njeopita- mzz-ir.mw
- v) a- *li*- chot- a
 nfs3um- njeopita- mzz- ir.mw
- vi) wa- *li*- imb- a
 nfs3wi- njeopita-mzz- ir.mw

Mofu njeo hii katika vitenzi haina mabadiliko yanayotokea kutokana na mfuatano wa irabu katika mzizi wa kitenzi.

Mofu njeo {-*ku*-}

Mofu njeo {-*ku*-} ya wakati uliopita ni mofu kanushi. Mofu hii huchukua nafasi ya mofu njeo yakinishi {-*li*-} ya wakati uliopita kama inavyoonekana katika Mfano 40 chini.

Mfano: 40

- i) si + ni-*li*-andika > si-*ku*-andika
- ii) ha + u-*li*-chuma > hu-*ku*-chuma
- iii) ha-a-*li*-cheza > ha-*ku*-cheza
- iv) ha + tu-*li*-iba > ha-tu-*ku*-iba
- v) ha + m-*li*-chota > ha-m-*ku*-chota
- vi) ha + wa-*li*-imba > ha-wa-*ku*-imba

Mofu njeo kanushi ya wakati uliopita {-ku-} katika Mfano 40 juu inaonekana kuchukua nafasi mofu njeo {-li-}.

4.3.1.1 Nafasi ya Mofu Njeo ya Wakati Uliopita Katika Kitenzi cha Kiswahili

Mofu njeo ya wakati uliopita katika kitenzi cha Kiswahili hutokea kati ya mofu nafsi na mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali cha pili baada ya kiambishi awali cha kwanza ambacho ni mofu nafsi. Mofu njeo {-li-} hujitokeza katika nafasi hii kama ifuatavyo:

Mofu njeo {-li-} katika kitenzi

Mfano: 41

- i) ni- li- chot- a
nfs 1um- njeopita- mzz- ir.mw
- ii) tu- li- chot- a
nfs 1wi-njeopita- mzz- ir.mw
- iii) u- li- chum- a
nfs2um- njeopita- mzz- irabu mw
- iv) m- li- chum- a
nfs2wi-njeopita- mzz- ir.mw
- v) a- li- ib- a
nfs 3um-njeopita- mzz- ir.mw
- vi) wa- li- imb-a
nfs 3wi- njeopita- mzz- ir.mw

Katika mifano hii tunaona nafasi ya mofu njeo {-li-} ya wakati uliopita inatokea baada ya mofu nafsi na kabla ya mzizi wa kitenzi katika umoja na wingi.

Mofu njeo {-ku-} ya wakati uliopita hutokea baada ya mofu kanushi kama Mfano: 42 (i, ii na iii) hapo chini unavyoonyesha.

Nafasi ya mofu njeo kanushi katika kitenzi

Mfano: 42

i) si- ku- fung- a

kan/nfs1-jeopita- mzz- ir.mw

ii) hu- ku- ib- a

kan/nfs2- njeopita- mzz- ir.mw

iii) ha- ku- chez- a

kan/nfs3- njeopita- mzz- ir.mw

iv) ha- tu- ku- fung- a

kan- nfs1 wi- njeopita- mzz- ir.mw

v) ha- m- ku- ib- a

kan- nfs2 wi- njeopita- mzz- ir.mw

vi) ha- wa- ku- chez- a

kan- nfs 3 wi- njeopita- mzz- ir.mw

Aidha mofu njeo {-ku-} hutokea pia baada ya mofu nafsi katika nafsi ya kwanza, pili na tatu wingi kama katika mfano wa namba 42 (iv, v na vi) hapa juu.

Katika mifano hii ya vitenzi, mofu njeo {-ku-} inaonekana kabla ya mzizi wa kitenzi baada ya mofu kanushi katika nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu umoja,

lakini inaonekana baada ya mofu nafsi katika nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu wingi na kabla ya mzizi wa kitenzi. Kutokana na hali hii mofu njeo {-ku-} katika vitenzi vyenye mofu kanushi hutokea baada ya mofu kanushi. Katika umoja Mfano 42 i) - iii) mofu kanushi hizi {si-, hu- na ha-} zimechukua nafasi na dhima ya mofu nafsi kama katika Mfano 42 i), ii) na iii). Halikadhalika hutokea baada ya mofu nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili wingi na nafsi ya tatu wingi {-tu-, -m- na -wa-} kama katika Mfano 42 iv), v) na vi).

4.3.2 Mofu Njeo za Wakati Uliopo (Njeopo)

Mofu njeo wakati uliopo katika Kiswahili inaelezea tendo linavyofanyika au halifanyiki wakati ule ule. Kwa hiyo tukisema `ninapika` tunadokezwa kuwa tendo la kupika linaendelea kutendeka wakati wa kutolewa kwa taarifa.

Mofu njeo katika vitenzi kwa wakati uliopo ni: {-na-} katika yakinishi na {-i} katika kanushi.

Mofu njeo katika yakinishi ni: {-na-}

Mfano: 43

- i) ni- na- chot-a
nfs 1um- njeopo- mzz- ir.mw
- ii) tu- na- chot- a
nfs 1wi- njeopo- mzz- ir.mw
- iii) u- na- chot-a
nfs 2um- njeopo- mzz -ir.mw
- iv) m- na- chot- a

nfs 2wi - njeopo- mzz- ir.mw

v) a- *na-* chot- a

nfs 3um- njeopo- mzz- ir.mw

vi) wa- *na-* chot- a

nfs 3wi- njeopo- mzz- ir.mw

Mofu njeo ya wakati uliopo inapoambishwa katika kitenzi hakuna mabadiliko yoyote kama katika mfano 44. Mofu njeo kanushi {-i} inapoambishwa katika kitenzi, hutokea mwishoni mwa kitenzi na kuchukua nafasi ya irabu mwisho.

Mfano: 44

i) si-chek- *i*

ii) ha-tu-chek- *i*

iii) hu-chek- *i*

iv) ha-m-chek-*i*

v) ha-chek-*i*

vi) ha-wa-chek-*i*

Mofu kanushi inapoambishwa katika kitenzi cha wakati uliopo mofu njeo {-na-} hudondoshwa na mofu njeo hii {-na-} dhima yake huchukuliwa na mofu njeo kanushi {-i} ambayo huchukua nafasi ya kiambishi tamati baada ya mzizi.

4.3.2.1 Nafasi ya mofu njeo ya wakati uliopo katika kitenzi cha Kiswahili

Mofu njeo ya wakati uliopo katika kitenzi cha Kiswahili hutokea kati ya mofu nafsi na mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali cha pili baada ya kiambishi awali cha kwanza ambacho ni mofu nafsi.

Mfano: 45

ni-*na*-chota

tu-*na*-chota

u-*na*-chota

m-*na*-chota

a-*na*-chota

wa-*na*-chota

Katika mfano huu, mofu njeo {-*na*-} ya wakati uliopo hutokea baada ya mofu nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu umoja na wingi na huwa kabla ya mzizi wa kitenzi.

Mofu njeo kanushi {-*i*} ya wakati uliopo hutokea mwishoni mwa kitenzi kama kiambishi tamati baada ya mzizi.

Mfano: 46

ni-*na*-enda > si-end-*i*

tu-*na*-enda > ha-tu-end-*i*

u-*na*-enda > hu-end-*i*

m-*na*-enda > ha-m-end-*i*

anaenda > ha-end-*i*

wa-*na*-enda > ha-wa-end-*i*

Katika mfano huu tunaona kuwa kitenzi *enda* kilipokanushwa, kimeambisha mofu njeo /i/ mwishoni kama kiambishi tamati na kuchukua nafasi ya irabu mwisho /a/.

Isitoshe, /a/ ilipoambishwa katika kitenzi chenye mofu njeo ya wakati uliopo, mofu hii ilidondoshwa. Hii ina maana kuwa mofu njeo {-na-} haikai pamoja na mofu kanushi katika kitenzi. Kwa mantiki hii ni dhahiri kuwa {-i} nayo ni mofu njeo ya wakati uliopo yenye kukanusha tendo linalotajwa katika wakati uliopo. Kwa hivyo, twaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa vitenzi vyote vyenye mofu njeo ya wakati uliopo {-na-} na kwa nafsi zote, vinapokanushwa huchukua mofu njeo {-i}. Kutokana na muktadha huu {-i} ni mofu njeo kanushi ya wakati uliopo.

4.3.3 Mofu Njeo za Wakati Ujao (Njeojao)

Mofu njeo wakati ujao hueleza tendo ambalo litafanyika wakati wote ujao baada ya mazungumzo. Wakati ujao una mofu njeo moja tu {-ta-} kama vile:

Mfano: 47

i) ni- ta- shind- a
nfs 1um- njeojao- mzz- ir.mw

ii) u- ta- rud- i
nfs 2 um-njeojao-mzz- ir.mw

iii) a- ta- pand- a
nfs3 um-njeojao-mzz- ir.mw

iv) tu- ta- palili- a
nfs1wi- njeojao- mzz- ir.mw

v) m- ta- chagu- a
nfs 2wi- njeojao- mzz- ir.mw

vi) wa- ta- onj- a
nfs3 wi- njeojao- mzz- ir.mw

Mofu njeo ya wakati ujao hutumika pia pamoja na vitenzi vilivyoambishwa mofu kanushi.

Mfano: 48

- i) si- ta- shind- a
 kan / nfs1um- njeojao- mzz- ir.mw
- ii) ha- tu- ta- shind- a
 kan- nfs1wi- njeojao- mzz- ir.mw
- iii) hu- ta- lim- a
 kan/nfs 2 um- njeojao- mzz- ir.mw
- iv) ha- m- ta- shind- a
 kan- nfs 2 wi- njeojao- mzz- ir- mw
- v) ha- ta- shind-a
 kan/nfs 3 um- njeojao- mzz- ir-mw
- vi) ha- wa- ta- shind- a
 kan - nfs 3 wi- njeojao- mzz- ir.mw

Kutokana na mifano hii ni dhahiri kuwa mofu njeo {-ta-} katika vitenzi haiathiri maumbo mengine yanayoambatana nayo.

4.3.3.1 Nafasi ya Mofu Njeo ya Wakati Ujao Katika Kitenzi cha Kiswahili

Mofu njeo ya wakati ujao katika kitenzi cha Kiswahili hutokea kati ya mofu nafsi na mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali cha pili baada ya kiambishi awali cha kwanza ambacho ni mofu nafsi. Mofu njeo inayotokea katika nafasi hii huwa ni vitenzi yakinishi.

Mfano: 49

- i) ni- *ta-* shind- a
nfs1um- njeopo- mzz- ir.mw
- ii) tu- *ta-* shind- a
nfs 1wi -njeopo-mzz- ir.mw
- iii) u- *ta-* rud- i
nfs 2 um- njeopo- mzz- ir.mw
- iv) m- *ta-* rud- i
nfs 2 wi- njeopo- mzz-ir.mw
- v) a- *ta-* pand-a
nfs 3um- njeopo- mzz- ir.mwi
- vi) wa- *ta-* pand- a
nfs 3wi- njeopo- mzz- ir.mw

Aidha, mofu njeo {-*ta-*} inapoambishwa pamoja na mofu kanushi katika kitenzi, hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi katika nafsi zote.

Mfano: 50

- i) si- *ta-* shind-a
kan/nfs1um- njeojao- mzz- ir.mw
- ii) ha- tu- *ta-* shind- a
kan- nfs1wi- njeojao- mzz- ir.mw
- iii) hu- *ta-* chek- a
kan/nfs 2 um- njeojao- mzz- ir.mw
- iv) ha- m- *ta-* pik- a

kan- nfs2wi- njeojao-mzz-ir.mw

v) ha- *ta-* funik-a

kan/nfs 3 um-njeojao-mzz- ir.mw

vi) ha- wa- *ta-* chek- a

kan - nfs 3 wi- njeojao-mzz- ir.mw

4.3.4 Idadi ya mofu njeo za kitenzi cha Kiswahili

Kitenzi cha Kiswahili kina mofu njeo tano ambazo zimegawanyika katika nyakati zifuatazo: Wakati uliopita una mofu njeo mbili: {-li-} na {-ku-}. Wakati uliopo una mofu njeo mbili: {na} na {i}. Wakati ujao una mofu njeo moja ambayo ni {-ta-}.

4.3.5 Mazingira ya Mofu Njeo na Jinsi Inavyoathiriwa na Umbo la Kitenzi cha Kiswahili

Maumbo ya mofu njeo za vitenzi vya Kiswahili huathiriwa na mazingira ya vipashio vingine vilivyo katika vitenzi vinavyoambatana navyo.

Kama tulivyoeleza katika 4.3.1 umbo la mofu njeo {-li-} huathiriwa na mofu kanushi inayoanza mwanzoni mwa kitenzi kabla ya mofu nafsi ambapo mofu {-li-} hudondoshwa na mofu kanushi {-ku-} huchukua nafasi ya mofu {-li-}.

Mofu kanushi inapoambishwa kwenye kitenzi chenye mofu njeo {-li-} wakati uliopita hudondoka na mofu njeo {-ku-} hutokea.

Mfano: 51

i) si + ni-*li*-chek-a > si+*ku*-chek-a

ii) ha + u-*li*-cheka > hu + *ku*-cheka

iii) $ha + a-li-cheke > ha + ku-cheke$

iv) $ha + tu-li-cheke > ha + tu-ku-cheke$

v) $ha + m-li-cheke > ha + m-ku-cheke$

vi) $ha + wa-li-cheke > ha + wa-ku-cheke$

Katika Mfano 51 i)-iii) mofu nafsi ya kwanza, pili na tatu umoja {*ni-*, *u-* na *a-*} ambazo ni vipatanishi hudondoshwa. Kutokana na kudondoshwa kwa mofu nafsi, mofu kanushi {*si-* na *ha-*} huchukua nafasi katika nafsi ya kwanza, pili na tatu umoja. Hata hivyo, mofu kanushi {*ha-*} inapofuatana na irabu / *u* / ya nafsi ya pili umoja na irabu / *a* / ya nafsi ya tatu umoja, irabu / *a* / hiyo ya mofu kanushi hudondoshwa pia. Tumeona katika mifano hapo juu kuwa katika Kiswahili mofu kanushi wakati uliopita ni mofu njeo {-ku}.

Mofu kanushi inapoambishwa kwenye kitenzi chenye mofu njeo wakati uliopo, mofu njeo hutokea mwishoni mwa kitenzi.

Mfano: 52

i) $tupa > ni-na-tupa$.

ii) $si-na-tupa > si-tup-i$

iii) $ha-u-na-tupa > hu-tup-i$

Katika mfano huu, tunaona kitenzi “tupa” kikiambishwa mofu njeo wakati uliopo na mofu nafsi. Halafu tunaona mofu kanushi ikiambishwa katika kitenzi chenye mofu njeo wakati uliopo. Matokeo yake ni kudondoshwa kwa mofu njeo {-na-} na kuingia kwa mofu njeo {-i} katika kitenzi hicho japokuwa kina kuwa katika nafasi tofauti.

Katika 4.3.3 tulijadili na kueleza jinsi maumbo ya mofu njeo za vitenzi vya Kiswahili yanavyojitokeza katika mazingira yanayoambatana nayo. Mofu njeo ya wakati ujao {-ta-} kama tulivyoona katika vitenzi haisababishi athari yoyote kwa maumbo mengine yanayoambatana nayo.

Mfano: 53

- i) *nitapika* > *sinitapika* > *sitapika*
- ii) *utapika* > *hautapika* > *hutapika*
- iii) *atapika* > *haatapika* > *hatapika*
- iv) *tutapika* > *hatutapika* > *hatutapika*
- v) *mtapika* > *hamtapika* > *hamtapika*
- vi) *watapika* > *ha-wa-ta-pika* > *hawatapika*

Katika mfano huu, tunaona kitenzi 'pika' kikiambishwa mofu njeo wakati ujao na mofu nafsi. Halafu tumeona mofu kanushi ikiambishwa katika kitenzi chenye mofu njeo wakati ujao. Matokeo yake ni kuwa mofu njeo {-ta-} katika kitenzi haileti mabadiliko yoyote yanavyojitokeza kwenye mofu kanushi.

4.4 Kulinganisha mofu njeo za Kikara na Kiswahili

Utafiti huu kama ilivyokwisha kuelezwa ulikusudia kulinganisha mofu njeo za Kikara na za Kiswahili ili kujua nafasi yake katika vitenzi vya lugha hizi, idadi yake na mazingira zinapotokea. Tumechunguza nafasi ya mofu njeo za vitenzi vya Kikara na Kiswahili katika 4.2.1 na 4.3.0, idadi ya mofu za vitenzi vya Kikara na Kiswahili katika 4.2.4.0 na 4.3.4.0 na mazingira ya mofu njeo na jinsi inavyoathiriwa na umbo la kitenzi cha Kikara na cha Kiswahili katika 4.2.5.0 na 4.3.5.0 kwa mfuatano huo.

Tumechunguza na kuchambua athari ya umbo la mofu njeo inayotokana na mazingira ilimo, yaani jinsi umbo la irabu ya mzizi wa kitenzi linavyoathiri umbo la mofu inayopakana na mzizi wa kitenzi husika. Katika kulinganisha mofu njeo za Kikara na Kiswahili tunatalii vipengele vyote vilivyotajwa juu na kuona jinsi lugha hizi zinavyofanana au kutofautiana katika uwasilishaji wa mofu njeo katika vitenzi vya lugha hizi.

4.4.1 Nafasi ya mofu njeo katika kitenzi cha Kikara na Kiswahili

Katika 4.2.1.1 tumeona kuwa mofu njeo za wakati uliopita kitambo zinatokea baada ya mzizi wa kitenzi cha Kikara kama kiambishi tamati ilihali katika 4.3.1 tuliona kuwa mofu njeo katika Kiswahili inatokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali.

**Jedwali 4.2: Nafasi za Mofu Njeo Za Kitenzi Cha Kikara Na Kiswahili
Zinapotokea Wakati Uliopita**

	Kikara	Kiswahili
i	na-kam-ile	ni-li-kama
ii	cha-sek-ele	tu-li-chek-a
iii	wa-ma-liny-a	u-li-pand-a
iv	mwa-me-ny-a	m-li-chez-a

Chanzo: Uchambuzi wa Data za utafiti

Ulinganishaji huu unaonyesha kuwa mofu njeo za wakati uliopita katika lugha hizi zinatokea katika nafasi tofauti za vitenzi. Katika 4.2.2 tumeona pia kuwa mofu njeo za wakati uliopo katika Kikara hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali na katika Kiswahili tumeona katika 4.3.2 mofu njeo hutokea kabla ya mzizi kama kiambishi awali.

Mazingira ya mofu njeo za wakati uliopo katika kitenzi kwa lugha hizi yanafanana katika nafasi zinamotokea Kikara {-e-} na Kiswahili {-na-}. Mofu njeo zote hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali.

4.4.1.1 Kufanana kwa Lugha Hizi

Tunapochunguza nafasi ya mofu njeo za kitenzi cha Kikara na Kiswahili wakati uliopo, tunabaini kuwa hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali kwa lugha zote.

Jedwali 4.3: Nafasi ya Mofu Njeo za Kitenzi cha Kikara na Kiswahili Wakati Uliopo

	Kikara yakinishi	Kiswahili yakinishi
i	ch- <i>e</i> -nok-a	tu- <i>na</i> -chum-a
ii	<i>e</i> -um-a	a- <i>na</i> -ham-a
iii	w- <i>e</i> -kweny-a	u- <i>na</i> -chez-a
iv	β- <i>e</i> -kwanj-a	wa- <i>na</i> -tandik-a

Chanzo: Uchambuzi wa Data za utafiti

Mazingira ya kutokea kwa mofu njeo za wakati uliopo katika kitenzi hufanana baina ya lugha hizi. Katika Kikara mofu njeo {-e-} hutokea baada ya mofu nafsi na mofu njeo ya Kiswahili {-na-} pia hutokea baada ya mofu nafsi

(a) *Kufanana kwa lugha hizi katika uyakinishi wakati ujao*

Wakati ujao lugha ya Kikara inafanana na Kiswahili katika nafasi zinapotokea katika kitenzi chenye mofu ya uyakinishi.

Jedwali: 4.4: Kufanana kwa Nafasi za Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili**Wakati Ujao**

	Kikara	Kiswahili
i	ni- <i>li</i> -um-a	ni- <i>ta</i> -ham-a
ii	a- <i>ka</i> -um-e	a- <i>ta</i> -ham-a
iii	we- <i>ndo</i> -um-a	u- <i>ta</i> -ham-a

Chanzo: Uchambuzi wa Data za utafiti

Mazingira ya mofu njeo za wakati ujao katika kitenzi kwa lugha hizi yanafanana katika nafasi zinamotokea.

- i) Mofu njeo ya lugha hizi hufanana katika nafasi zinamotokea, hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi na baada ya mofu nafsi katika kitenzi.
- ii) Mofu njeo ya lugha hizi zote hutokea kama viambishi awali.
- iii) Mofu njeo ya lugha hizi hutokea katika mazingira yanayofanana.

(b) *Kufanana kwa lugha hizi katika ukanushi wakati ujao*

Mofu njeo za Kikara na Kiswahili zinatokea katika nafasi sawa kwa nafsi ya 1, 2 na 3 wingi wakati ujao.

Jedwali 4.5: Kufanana kwa Nafasi za Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili**Wakati Ujao Mofu Kanushi**

	Kikara ukanushi	Kiswahili ukanushi
i	m-ta- <i>ka</i> -laβ-e	ha-m- <i>ta</i> -onj-a
ii	βa-ta- <i>ku</i> -laβ-a	ha-wa- <i>ta</i> -onj-a
iii	chi-te- <i>ndo</i> -laβ-a	ha-tu- <i>ta</i> -onj-a

Chanzo: Uchambuzi wa Data za utafiti

- i) Mofu njeo hizi zote hutokea baada ya mofu kanushi katika nafsi ya kwanza, pili na tatu wingi.
- ii) Mofu njeo hizi zote hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi pia na ni kiambishi awali.
- iii) Mofu njeo ya lugha hizi hutokea katika mazingira yanayofanana. Katika jedwali 6, Kikara mofu njeo hutokea nafasi ya tatu kabla ya mzizi. Hii ni sawa na Kiswahili mofu njeo hutokea nafasi ya tatu kabla ya mzizi wa kitenzi.
- iv) Viambishi tamati katika lugha hizi mbili huishia irabu / a / katika wakati ujao isipokuwa wakati ujao kitambo kiasi katika Kikara huishia irabu / e / kwa sababu ya usawazisho wa matamshi

4.4.1.2 Kutofautiana kwa lugha hizi

Tunapolinganisha nafasi ya mofu njeo za kitenzi cha Kikara na Kiswahili wakati uliopo katika mofu kanushi, hutokea katika nafasi tofauti.

Jedwali 4.6: Tofauti ya Nafasi ya Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Wakati

Uliopo Mofu Kanushi

	Kikara kanushi	Kiswahili kanushi
i	chi-t- <i>e</i> -nok-a	ha-tu-chum- <i>i</i>
ii	βa -t- <i>e</i> -um-a	ha-wa-ham- <i>i</i>

Chanzo: Uchambuzi wa Data za utafiti

- i) Katika Kikara mofu njeo hutokea baada ya mofu kanushi na kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali.
- ii) Katika Kiswahili mofu njeo kanushi hutokea mwishoni mwa kitenzi kama kiambishi tamati.

Kwa hali hii mofu njeo {-i} ni mofu njeo pekee ya Kiswahili ambayo hutokea katika nafasi tofauti na mofu njeo nyingine. Mofu njeo {-i} ina dhima 2 ambazo ni kuwa: a) kiambishi tamati na b) mofu kanushi ya wakati uliopo Taz. Jedwali 7 hapo juu.

Mofu njeo za Kikara na Kiswahili zinatokea pia katika nafasi tofauti kwa nafsi ya 1, 2 na 3 umoja wakati ujao. Jedwali lifuatalo linaonyesha tofauti ya nafasi ya mofu njeo za Kikara na Kiswahili zinapotokea.

Jedwali 4.7: Tofauti ya Nafasi ya Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Wakati

Ujao Mofu Kanushi

	Kikara ukanushi	Kiswahili ukanushi
i	ni-ta-ka-laß-e	si-ta-onj-a
ii	u-ta-ku-laß-a	hu-ta-onj-a
iii	a-te-ndo-laß-a	ha-ta-onj-a

Chanzo: Uchambuzi wa Data za utafiti

Kutokana na jedwali hili tunaona kuwa mofu njeo za Kikara hutokea katika nafasi tofauti katika nafsi ya 1, 2 na 3 umoja. Mofu njeo za Kikara hutokea baada ya mofu kanushi kabla ya mzizi wa kitenzi ilhali mofu njeo ya Kiswahili hutokea baada ya mofu kanushi ambazo pia zina dhima ya mofu nafsi.

Aidha, kiambishi tamati cha kitenzi chenye mofu njeo ya wakati ujao kitambo kiasi katika Kikara huishia irabu / e / ilhali Kiswahili huishia irabu / a /.

4.4.2 Idadi ya mofu njeo za Kikara na Kiswahili

Kama tulivyoeleza katika 4.2.4.0 juu, Kikara kina jumla ya mofu njeo saba na Kiswahili kina mofu njeo tano kama ilivyoelezwa katika 4.3.4.0.

Mofu njeo za wakati uliopita za Kikara na Kiswahili

Kikara kina mofu njeo za wakati uliopita mbili: {-ile-} na {-ma-} ambazo zote hutumika katika uyakinifu na ukanushi. Katika Kiswahili mofu njeo za wakati uliopita ni mbili pia, {-li-} na {-ku-} ambayo ni mofu kanushi.

Jedwali 4.8: Idadi ya Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Katika Wakati Uliopita

Kikara	Mofu njeo	Kiswahili	Mofu njeo
na-kam-ile	-ile	ni-li-kam-a	-li-
ni-ta-kam-ile	-ile	si-ku-kam-a	-ku-
ch-eny-ele	-ele	tu-li-chez-a	-li-
mwa-ma-sol-a	-ma-	m-li-chagu-a	-li-
m-ta-ma-sol-a	-ma-	ha-m-ku-chagu-a	-ku-
mwa-me-timb-a	-me-	m-li-simam-a	-li-

Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti

Hivyo basi, jedwali hili linaonyesha kuwa Kikara kina mofu njeo mbili za wakati uliopita zenye umbo tofauti na Kiswahili pia kina mofu njeo mbili za wakati uliopita zenye umbo tofauti.

Mofu njeo za wakati uliopo za Kikara na Kiswahili

Wakati uliopo katika Kikara una mofu njeo moja {-e-} ilhali Kiswahili kina mofu njeo mbili {-na-} na {-i-}.

Jedwali lifuatalo linaonyesha idadi ya mofu njeo za Kikara na Kiswahili katika wakati uliopo.

Jedwali 4.9: Idadi ya Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Wakati Uliopo

Kikara	Mofu njeo	Kiswahili	Mofu njeo
mw-e-sol-a	-e-	m-na-chagu-a	-na-
m-t-e-sol-a	-e-	ha-m-chagu-i	-i-

Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti

Kutokana na jedwali hili tunaona kuwa Kikara kina mofu njeo moja na Kiswahili kina mofu njeo mbili zenye maumbo tofauti katika wakati uliopo.

Mofu njeo za wakati ujao za Kikara na Kiswahili

Wakati ujao katika Kikara una mofu njeo nne: {-li-}, {-ka-, -ke-}, {-ndo-} na {-ku-} na Kiswahili kina mofu njeo moja: {-ta-}.

Jedwali 4.10: Idadi ya Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili Wakati Ujao

Kikara	mofu njeo	Kiswahili	mofu njeo
m-li-suuk-a	-li-	m-ta-fufuk-a	-ta-
a-ka-suuk-e	-ka-/ ke-	a-ta-fufuk-a	-ta-
u-ta-ku-suuk-a	-ku-	hu-ta-fufuk-a	-ta-
βe-ndo- suuk-a	-ndo-	wa-ta-fufuk-a	-ta-

Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti

Kwa hivyo, wakati ujao katika Kikara una mofu njeo nne zenye maumbo tofauti kati ya hizi mofu {-ku-} ni kanushi na Kiswahili kina mofu njeo moja {-ta-}.

4.5 Hitimisho

Sura hii imejibu maswali yote manne ya utafiti. Maswali haya yalilandana na malengo ya utafiti na hivyo yalifafanuliwa kwa mawanda mapana.

Kwanza, tuliangalia nafasi ya mofu njeo katika kitenzi cha Kikara na kisha mofu njeo katika kitenzi cha Kiswahili. Tuliona kuwa katika Kikara nafasi ya mofu njeo moja hutokea baada ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi tamati na mofu njeo sita hutokea kabla ya mzizi kama kiambishi awali. Katika Kiswahili tuliona pia kuwa

mofu njeo moja hutokea baada ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi tamati na mofu njeo nne hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi kama kiambishi awali.

Pili, tuliangalia idadi ya mofu njeo za lugha hizi mbili. Tuligundua kuwa Kikara kina mofu njeo saba: wakati uliopita una mofu njeo mbili, wakati uliopo una mofu njeo moja na wakati ujao una mofu njeo nne. Kiswahili kina mofu njeo tano: wakati uliopita una mofu njeo mbili, wakati uliopo una mofu njeo mbili na wakati ujao una mofu njeo moja.

Tatu, tuliona maumbo ya mofu njeo ya Kikara yanavyoathiriwa katika kitenzi pale ambapo irabu inapokuwa katika mzizi wa kitenzi au irabu inaanza mwanzoni mwa kitenzi. Katika Kiswahili tuliona kuwa mofu njeo ya wakati uliopita mofu njeo yakinishi hudondoshwa katika ukanushi na wakati uliopo yakinishi hutokea baada ya mofu njeo hii kudondoshwa na mofu njeo ya wakati uliopo kitenzi kanushi hutokea mwishoni mwa kitenzi.

Nne, mofu njeo za Kikara na za Kiswahili tulilinganisha katika nafasi, idadi na kuona mazingira zinamotokea. Katika kulinganisha tulibaini kuwa nafasi za mofu njeo za lugha hizi kuna kufanana na kutofautiana, pia katika idadi tuligundua kuwa idadi za mofu njeo hizi zinatofautiana na katika mazingira zinamotoka tulibaini kuwa mofu njeo hizi baadhi zinatokea katika mazingira yanayofanana na zingine yanayotofautiana.

SURA YA TANO

5.0 MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti unaoweza kufanywa na wanazuoni wengine. Sura hii imegawanyika katika sehemu tatu: Sehemu ya kwanza inaelezea muhtasari wa matokeo ya utafiti huu, sehemu ya pili ni mapendekezo na sehemu ya tatu ni hitimisho la utafiti huu.

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza, kubaini na kulinganisha mofu njeo za Kikara na za Kiswahili ili kujua nafasi, idadi yake na mazingira zinapotokea. Utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi manne: Kwanza kuchunguza nafasi ya mofu njeo katika kitenzi cha Kikara na cha Kiswahili ili kuona mazingira zinamotokea. Pili, kuchunguza idadi ya mofu njeo za Kikara na za Kiswahili ili kubaini iwapo ni sawa au la. Tatu, kuchunguza mazingira ya mofu njeo na jinsi inavyoathiriwa na umbo la kitenzi ambamo mofu inatokea. Nne, kulinganisha mofu njeo za Kikara na Kiswahili ili kuona iwapo zinatokea katika nafasi ile ile au la. Utafiti huu ulijibu maswali ya utafiti ambayo yalikusudiwa kutupatia data tuitakayo.

Utafiti huu ulifanyika kata ya Bukiko na Nyamanga katika wilaya ya Ukerewe mkoa wa Mwanza. Utafiti huu, ulichunguza na kulinganisha mofu njeo za Kikara na za Kiswahili ili kujua nafasi, idadi yake na mazingira zinapotokea. Utafiti huu ulitumia watafitiwa 45 waliotumika kama sampuli ya utafiti huu. Mbinu zilizotumika katika

kukusanya data za utafiti huu ni usaili na dodoso. Utafiti huu ulitumia mkabala wa uwandani na maelezo katika ukusanyaji wa data. Katika utafiti huu, mtafiti amegundua kwamba, baadhi ya mofu njeo za Kikara na Kiswahili zinatofautiana, zipo zinazotokea kabla ya mzizi wa kitenzi ambazo ni wakati uliopita wa karibu {-ma-/me-}, wakati uliopo {-e-}, wakati ujao kitambo {-li-}, wakati ujao kiasi {-ka-/ke-}, {-ku-/kw-} wakati ujao wa karibu {-ndo-} katika Kikara wakati uliopita {-li-}, {-ku-}, wakati uliopo {-na-} yakinishi, wakati ujao {-ta-} katika Kiswahili na zinazotokea baada ya mzizi wa kitenzi ambazo ni: mofu njeo {-ile/ -ele} katika Kikara na {-i} katika Kiswahili. Pia kuna zinazofanana ambazo hutokea nafasi ya (2) ambazo ni: {-ma- / -me-}, {-e-}, {-li-, -ka-/ke-, -ndo-} za Kikara {-li-, -ku-}, {-na-}, {-ta-} za Kiswahili, lugha zote ni katika uyakinishi au nafasi ya (3) baada ya mofu nafsi kanushi kabla ya mzizi wa kitenzi ambazo ni: {-ma- / -me-}, {-e-}, {-li-, -ka-/ke-, -ku-/kw-, -ndo-} za Kikara, {-ku-}, {-ta-} Kiswahili katika nafsi ya kwanza, pili na tatu wingi tu. Kwa mfano Kikara kina mofu njeo moja {-ile/-ele} inayotokea baada ya mzizi wa kitenzi na Kiswahili kina mofu njeo moja pia {-i} inayotokea baada ya mzizi. Aidha, tumeweza kugundua kuwa mofu njeo za Kikara na za Kiswahili zinatofautiana kiidadi. Kikara kina mofu njeo saba ambazo zinatokana na aina tatu ambazo ni: mofu njeo ya wakati uliopita ambao una viwango viwili vya wakati uliopita: mofu njeo wakati uliopita kitambo unaobainishwa maumbo mawili {-ile / -ele}, mofu njeo ya wakati uliopita wa karibu unaobainishwa na maumbo mawili {-ma-/me-}. Kundi la pili ni wakati uliopo ambalo hubainishwa na mofu njeo {-e-} na kundi la tatu ni wakati ujao ambao una viwango vitatu vya wakati ambavyo ni: wakati ujao kitambo unaobainishwa na mofu njeo {-li-}, wakati ujao kitambo kiasi unaobainishwa na mofu njeo mbili {-ka- / -ke-} na {-ku-} na wakati ujao wa karibu

unaobainishwa na mofu njeo {-ndo-} ilihali Kiswahili kina mofu njeo tano ambazo zimegawanyika katika nyakati zifuatazo: wakati uliopita una mofu njeo mbili: {-li-} na {-ku-}, wakati uliopita una mofu mbili: {-na-} na {-i-} na wakati ujao una mofu njeo moja: {-ta-}. Vilevile, tumeweza kuthibitisha kuwa athari zinazotokea katika lugha ya Kikara husababishwa na muungano wa irabu zinazokabiliana katika kingo zake na athari zinatokea katika lugha ya Kiswahili katika mofu ukanushi pale ambapo mofu njeo {-li-} yakinishi na {-na-} yakinishi hudondoka na mofu njeo {-ku-} na {-i-} huchukua nafasi.

5.3 Mchango wa Utafiti

Katika utafiti huu tumeona kuwa japokuwa mofu njeo za Kiswahili zimeainishwa na wanazuoni kadha kama Mgullu (2011) Habwe na Karanja (2007) Wesana- Chomi (2001 na 2003) tumebaini mapungufu ambayo yalihatiji kuchunguzwa kwa kina zaidi. Mofu njeo za Kikara hazijachunguzwa kabisa. Utafiti wa Walker (2013), ulichunguza lugha za kundi moja ambazo zote ni za mkoa wa Mara na kuzilinganisha na Kiswahili na Kiingereza. Isitoshe, hakuna uchunguzi uliofanywa kwa lugha za Kibantu za makundi tofauti ambazo hazina toni, mathalani Kiswahili na Kikara. Kwa kuwa lugha za Kibantu zinatofautiana, ilionekana kuwa kulinganisha mofu njeo za lugha ya Kikara na Kiswahili ni muhimu kwa vile ni eneo ambalo halijachunguzwa bado.

5.4 Mapendekezo ya Tafiti Zijazo

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu tunapendekeza uchunguzi zaidi wa mofu mbalimbali za kitenzi cha Kikara. Kwa kuwa utafiti huu ulichunguza mofu njeo peke

yake inapendekezwa kuwa tafiti zaidi zifanywe kuchunguza mofu nyingine ambazo hazijafanyiwa utafiti. Hivyo kuna haja ya kufanya tafiti katika kitenzi cha Kikara ambacho kina mofu nyingi ambazo hazijashughulikiwa kabisa kama vile mofu nafsi, mofu za ukanushi, mofu za hali, mofu za masharti, mofu za urejeshi, mofu yambwa, na nyingine. Vilevile kuna haja ya kufanya utafiti wa kulinganisha mfumo katika kitenzi cha lugha ya Kikara (kiregi), Kijita, Kiruri na Kikwaya ambazo zipo katika kundi moja E. 25 Suguti. Aidha, hadi tunakamilisha kazi hii ya utafiti hatujapata maandiko maalumu ya kutosha ya kiisimu kuhusiana na lugha hii ya Kikara (Kiregi). Kwa mantiki hiyo kuna haja ya kujitoa kwa hali na mali ili kuchunguza maeneo mengine ya kitaalamu juu ya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantikia ya lugha ya Kikara.

5.5 Hitimisho

Sura hii imeeleza kwa muhtasari utafiti huu kwa kueleza malengo ya utafiti, mbinu za utafiti zilizotumiwa, eneo ambapo utafiti huu umefanyika pamoja na nadharia iliyotumika katika kuchambua data hii. Aidha uchambuzi wa data umeelezwa ukibainisha jinsi malengo ya utafiti yalivyofikiwa na mapendekezo ya utafiti zaidi katika maeneo ambayo mtafiti hajayashughulikia. Katika utafiti huu tumeonyesha jinsi mofu njeo za vitenzi vya lugha za Kikara na Kiswahili zinavyofanana na kutofautiana katika idadi yake, nafasi yake katika kitenzi, mazingira ya kutokea kwake na jinsi mazingira hayo yanavyoathiri maumbo ya mofu njeo kwa nafasi za mofu njeo zinapotokea. Aidha katika utafiti huu tulithibitisha athari zinazotokea usababishwa na irabu zinapokabiliana na irabu.

MAREJEO

- Beaudoin-Lietz, C. A. M. (1999). *Formatives of Tense, Aspect, Mood and Negation in the Verbal Construction of Standard Swahili*. Doctoral thesis, Memorial University of Newfoundland.
- Besha, R. M. (1985). *A study of Tense and Aspect in Shambala*. Unpublished PhD Thesis, Dar es Salaam: University of Dar es Salaam, Tanzania.
- Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Comrie, B. (1985). *Tense*. Cambridge: CUP.
- Crystal, D. (1991). *The Penguin Dictionary of Language*. London: Penguin Books.
- González, P. (2003). *Aspects on Aspect: Theory and Applications of Grammatical Aspect in Spanish*. PhD Dissertation. Ohio: Ohio State University, USA.
- Guthrie, M. (1948). *The Classification of Bantu Language*. London: Oxford University Press.
- Habwe, J. & Karanja, P. (2007). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Johnson, M. R. (1977). *A Semantic Analysis of Kikuyu Tense and Aspect*. Ohio State University. Retrieved from https://etd.ohiolink.edu/!etd.send_file.../ on 16th May, 2015.
- Katamba, F. & Stonham, J. (2006). *Morphology*. London: Palgrave Macmillan.
- Kombo, K. D. & Tromp, A. L. D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Makuyu: Don Bosco Printing Press.
- Kothari, C. R (2004). *Research methodololgy: methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Ltd.

- Lindfors, A. L. (2003). *Tense and Aspect in Swahili*. Institutionen for Lingvistik, Uppsalla Universitet. Uppsala, Sweden. Retrieved 22nd September, 2015 from www2.lingfil.uu.se/ling/semfiler/Swa_TAM.pdf.
- LOT (2009). *Atlas ya Lugha za Tanzania*. Language of Tanzania Project. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam, Tanzania.
- Marealle, I. B. (1978). *Dhana ya Mofu, Mofimu na Alomofu*, katika Mulika na.13. Dar es Salaam: TUKI.
- Mdee, J. S. (1999). *Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press Ltd.
- Mekacha, R. D. K. (2000). *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*. Minocity: Osaka University of Foreign Studies.
- Mfaume, E. G. (1984). *Misingi ya Isimu ya Lugha ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Printpak (T) Ltd.
- Mgullu, S. R. (2011). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Kenya Ltd.
- Mligo, E. S. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti Yenye Mantiki*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGYS).
- Mreta, A. Y. (1998). *An Analysis of Tense and aspect in Chasu: Their Form and Meaning in the Affirmative Constructions*. Hamburg: LIT.
- Nurse, D. (2008) *Tense and Aspect in Bantu*. Oxford: Oxford University Press.
- Nurse, D. and Hinnebusch, J. T. (1993). *Swahili and Sabiki*: London: University of California Press, Ltd.
- O'Grady, W., Katamba, F. & Archibald, J. (1997). *Contemporary Linguistics: An Introduction*. New York: Pearson Education.

- Pratt, M. (1972). *Tone in Some Kikuyu Verbal Forms. Studies in African Languages* 3(3), 25-377. University of Illinois, Champaign-Urbana.
- Reichenbach, H. (1947). *Elements of Symbolic Logic*. New York: The Free Press.
- Rubanza, Y. I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Smith, C. S. (1978). The Syntax and Interpretation of Temporal Expressions in English. *Linguistics and Philosophy*. Vol. 2, 43-99. Retrieved on 11th May, 2015 from <http://link.springer.com/article/10.1007/BF00365130>.
- Walker, J. B. (2013). *Comparative Tense and Aspect in the Mara Bantu Languages: Towards a Linguistic History*. Unpublished Thesis of Master of Arts. Trinity Western University, British Columbia, Canada. Retrieved on 22nd June, 2015 from <http://arcabc.ca/islandora/object/twu%3A220>.
- Wesana-Chomi, E. (2001). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. African Studies Research Centre, Sebha, Libya.
- Wesana-Chomi, E. (2003). *Kozi Fupi Tangulizi katika Sarufi Maumbo ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Sebha, Libya.
- Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: DUP.

KIAMBATISHO

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

DODOSO HII INAHUSU UTAFITI LINGANISHI WA MOFU NJEO ZA KIKARA NA KISWAHILI

Mimi ni mwanafunzi January Peter Nyawema Magesa wa uzamili katika somo la Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Hivyo, ninakusanya taarifa hizi ili kuweza kukamilisha sehemu ya masomo yangu ambapo itatoa mchango katika kulinganisha lugha hizi mbili: Kikara na Kiswahili ili kuhifadhi na kuziendeleza. Taarifa zitakazotolewa ni siri na zitatumika kwa lengo la kukamilisha utafiti huu tu. Hivyo, nakuomba msaada wako wa kutoa taarifa hizi ili kufanikisha utafiti huu.

A.Taarifa za mtafitiwa.

Jinsia.....,umri.....,kata.....na kiwango cha elimu.....

Maswali kuhusu utafiti:

Tafadhali katika sehemu hii, unatakiwa kujibu maswali yote katika nafasi zilizowazi na hauruhusiwi kuandika jina lako.

1. Andika vitenzi vifuatavyo katika lugha ya Kikara.

Unacheka 'weseka' ulicheka 'wasekele' utacheka 'uliseka' walichagua 'βamasola' watachagua 'βakasole' wanachagua 'βesola' ninachuma 'nenoka' nilichuma 'namanoka' nitachuma 'nendonoka' atapalilia 'endosenja' alipalilia 'asenjele' anapalilia 'esenja' unasimama 'wekwitimβa' husimami 'utakwitimβa' utasimama 'ulitimβa' hutasimama 'utalitimβa' sikuchota 'nitamataya' hawakuchota 'βatamataya' hakuchota 'atamataya' mlimwaga 'mwamasuka' mtamwaga 'mwakasuke' hammwagi 'mtesuka' tulirudi 'chasuβile' tunarudi 'chesuβa' tutarudi

‘chendosuβa’ hatutashinda ‘chitalisinga’ hawatashinda ‘βatalisinga’ sitashinda ‘nilisinga’.

2. Katika sentensi za Kiswahili zifuatazo ziandikwe tena kwa lugha ya Kikara. Kwa kujaza nafasi zilizowazi.

a) Mama anafua nguo sasa hivi ziwani.

mai emota chiguβo oli anu kumwalo

b) Mama hafui nguo sasa hivi ziwani.

mai atemota chiguβo oli anu kumwalo

c) Mama hakufua nguo juzi ziwani

mai atamamota chiguβo echolila kumwalo

d) Mama alifua nguo juzi ziwani

mai amotele chiguβo echolila kumwalo.

e) Baba aliua nyoka juzi.

lata emeta ichoka echolilya.

f) Baba ataua chatu kesho kutwa.

lata akete isatu echolilya

g) Baba na bibi wanamua nyoka sasa hivi

laba na kaka βekwita ichoka oli anu

h) Yesu alifufuka siku ya tatu zamani

Yesu asuukile kulu siku lwa kasatu kala

i) Mimi nitafufuka siku ya mwisho

nilisuuka kulusiku lwa kuβutelo

j) Mpishi anaonja chukula jikoni

Omuteki elaba efilyo mwitekelo

k) Baba na bibi hawaonji chakula jikoni

lata na mai batelaba efilyo mwitekelo

l) Rafiki yangu hakuchuma kisamvu juzi

omusani wani atamanoka echisamu echolilya

m) Babu anapura mawe

chachi euula ofulo / ofufole

n) Bibi hapuri bali anapepete mawe sasa hivi

kaka ateuula ila egulusha ofulo oli anu.

o) Kesho nitavuna mahindi machache

p) *mutondo nakakese amalingwa matyali.*

3. Tafsiri sentensi zifuatazo za Kikara katika lugha ya Kiswahili.

i) Lata amaiβuma ing`a likolo

baba alimpiga ng`ombe jana.

ii) Lata atamaiβuma ing`a likolo

baba alimpiga ng`ombe jana.

iii) Sengi eteka echai mwitekelo oli

shangazi anapika chai jikoni sasa.

iv) Chachi endokwesa ichoka emwila

babu atamtupa nyoka porini.

v) Mkaye atakuola kulusiku lwo kumalisya.

Mke wake hatapona katika siku ya mwisho

vi) Echolilya katondo nitakamile ing`a ya mama

Juzi asubuhi sikukama ng`ombe wa mjomba.

vii) Nyamwelo akenye ompila akamenya ota amalobo

Nyamwelo atacheza mpira akiweza kupinda ndoano.

viii) Omsubati akaume omwaka okwo okwicha

dada atahama mwaka ujao.

ix) Omlaghana huo etile imbusi yani.

Kijana wako aliua mbuzi wangu.

x) Mukaani ekwanja oβulili oli esiko.

Mke wangu anatandika kitanda sasa chumbani

xi) Mukaani atekwanja oβulili oli esiko

Mke wangu hatandiki kitanda sasa chumbani

Vitenzi vya Kikara vilivyotumiwa katika utafiti huu ni:

anja (tandika), βuma(piga), enya (cheza), esa (tupa), gulusha(pepeta), ika(shuka), ita (ua), itimba (simama), kama(kama), kesa(vuna), laβa(onja), linya(panda), mota(fua), noka (chuma), ola (pona), ota(pinda),seka(cheka), senja(palilia), singa (shinda), sola (chagua), suβa(rudi), suka (mwaga), suuka(fufuka),taya(chota), teka (pika), uma(hama) na uula (pura).